# Nipashe

Jumanne Juni 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580605

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Korti** yaihoji Jamhuri kueleza sababu kesi ya Tundu Lissu kuchelewa

UKURASA 3

**Serikali** yaanika vipaumbele 13 vya ukuaji uchumi Mwaka wa Fedha 2021/22

UKURASA 5


Nipashe TESA

Jumanne Juni 8, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

'Kilichoua Ushirika ni hiki, mikakati kuuinua yatajwa'

Kiswahili Pwani VS Maziwa Makuu

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

COVID-19 inavyozidi kuumiza waathirika wa udhalilishwaji

UKURASA 11

# Uchaguzi wa kombinesheni wamuibua Waziri mtandaoni

• **Atumia** muda kuwajibu kwa mifano, wengi walio-jitokeza kueleza shida ziliko... *Endelea Uk.2*



Waziri Wizara ya Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu

## Samia afuta mashamba, awagawia wananchi

UKURASA 3



## Lowassa, Mbowe walivyomlilia TB Joshua

UKURASA 2

MICHEZO WACHEZAJI YANGA WAIANIKA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Uchaguzi wa kombinesheni wamuibua Waziri mtandaoni

**Na Waanndishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, juzi na jana alitumia mitandao yake ya kijamii kujibu malalamiko ya wazazi juu ya namna watoto wao walivyopangiwa tahasusi (combination).

Ummy (pichani) alijibu, huku wachangiaji wakitoa mifano ya watoto wao waliomaliza kidato cha nne mwaka jana kupangiwa wasichochagua.

Waziri huyo alilazimika kutoa ufafanuzi huo kwenye mtandao wa Facebook, Twiter na Instagram, kutokana na kuibuka malalamiko ya wanafunzi kupangiwa tahasusi ambazo hawakuchagua, baada ya wizara kutangaza majina ya wanafunzi waliochaguliwa kuendelea na kidato cha tano na vyuo mbalimbali, akisisitiza walipangwa kulingana na chaguo lao.

Waziri huyo alijibu malalamiko kwa kuonyesha jina la mwanafunzi alivyochagua kwenye mfumo husika na kuataka wazazi kufuatilia kwa karibu wanachojaza watoto wao.

Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Mtwara, alisema wizara inafikiria kuja na mpango wa kuwataka wazazi wenye watoto wanaotarajia kumaliza kidato cha nne, kuandika barua maalum ya tahasusi wanayopendekeza watoto wao wajaze kwa ajili ya kuondoa mkanganyiko kati ya wanafunzi na wazazi

Waziri Ummy alisema: "Mzazi ametuletea hoja kuwa kijana wake amechaguliwa PGM na kuwa chaguo la kwanza na pili, chaguo la tatu na nne ni PCM na EGM. Tumekwenda kucheck (kuangalia) taarifa zake kwenye mfumo. Kijana chaguo la kwanza kajaza PGM. PCM ni chaguo la tano."

"Nilichobaini wazazi/walezi wengi wanatofautiana mtazamo na watoto wao, hivyo watoto wanafanya 'selection' (uchaguzi) bila kuwashirikisha wazazi.

Kulwa Jr aliandika "Mnakosea kuwapangia watoto vyuo angali wazazi wao hana pesa za kuwapeleka huko, nina ndugu yangu ana daraja la kwanza kwa alama 10 cha kushangaza kapeleka kusoma diploma ya 'Automobile 'Engineering' mtoto wa kike, haya mambo ya diploma angalieni wenye ufaulu mdogo au wanaohitaji."

Naye, Zaina Bakari aliandika "Kuna kijana kamaliza Mzumbe, Anuay Boimanda, kapata daraja la kwanza kwa alama tisa, aliomba PCB Mzumbe kwenye machaguo yote matano, ila mmempangia shule inaitwa Sekondari ya Handeni ambayo hakuomba na ni shule ambayo hakuchagua, mtoto analia tu."

Rahma Suleiman aliandika: "Hii siyo mara ya kwanza kutokeea 2014/2015 kijana anafaulu vizuri, lakini masomo hayatengenezi tahasusi bado anachaguliwa kujiunga kusoma kidato cha tano na sita mwisho anazuiliwa kufanya mtihani sababu hakidhi vigezo kivipi? miaka miwili aliyopoteza!kuna haja ya kujitathmini hapa."

Naye JM aliandika na kutoa mfano wa kilichojazwa kwenye mfumo wa uchaguzi kuwa: "Naomba uangalie huyo mwanangu aitwaye Magadalena Bitungwa awali alichaguliwa kweda Songea Girls PCB, lakini mmebadilisha eti sasa aende Lukas Malia sababu nini hasa. Mtoto alishajiandaa kisaikolojia kwenda kusoma Songea ghafla anabadilishwa naomba sababu maana maneno yanasemwa."

Naye, Kyala Nkota aliandika: "Mwanangu alipata daraja la kwanza kwa alama tisa tahasusi ya PCB Minaki au Same Sekondari, lakini kachaguliwa kwenda Rujewa shule ambayo hataki maana hataki shule za mchanganyiko." Pia, katika ukurasa mwingine Waziri aliandika: "Mzazi analalamika kwa nini kijana wake hakupangwa hatasusi kulingana na ufaulu wake na sifa za kuchaguliwa kwenye tahasusi husika, Hata hivyo, zinaweza kuwepo 'genuine cases' tupo tayari kuzifanyia kazi."

Waziri Ummy aliandika " Moja ya mzazi aliyetutumia ujumbe kuwa kijana wake kachaguliwa HGK wakati kijana alijaza PCB. Tumerudi kwenye mfumo kuona chaguo la kwanza ni HGK shule Madibira, la pili HGK shule Mara, la tatu HGK shule Kigwe, la nne CBG shule Same na la tano HE shule Kibiti, mfumo umempatia chaguo lake la kwanza.


17:13

Tweet

Ummy Mwalimu
@ummymwalimu

Huyu 👇- mzazi analalamika kwa nini kijana wake hakupangwa combination ya sayansi. Mfumo umempatia tahasusi kulingana na ufaulu wake na sifa za kuchaguliwa kwenye combination husika. Hata hivyo zinaweza kuwepo genuine cases, tupo tayari kuzifanyia kazi #UchaguziForm5

:23 · 06 Jun 21 from Dar es Salaam, Tanzania · Twitter for iPhone

Retweets 7 Quote Tweets 302 Likes

Kiokote @ismailerick · 1d
Replying to @ummymwalimu
Kwanini tuwachagulie Vijana ni Cha Kusoma?Je ana interest na hicho ambacho mfumo umempangia?Mzazi ana haki ya kulalamika sababu anapolipa Ada anakuwa na ndoto mwanae afikie malengo flan katika Elimu yake,So tusiue ndoto za Vijana kwa kuwapangia Masomo wasiyokuwa na interest nayo.

Emmanuel Frank aliandika " Nimekutana na 'situation' (hali) ya kijana ambaye chaguo lake la kwanza lilikuwa PCB na la pili CBG Same Sekondari ila kachaguliwa CBG, je, anaweza kubadilisha katika shule hiyo maana ndoto yake ni kuwa daktari,?alihoji.

Katika ukurasa huo, Sule Msiagi aliandika: " Ni kweli mtoto wa dada yangu amepata daraja la kwanza lakini amepangia kwenda kusoma daktari msaidizi Bombo na alijaza hiyo kitu bila ya kubadili kwenda chuo badala ya kuendelea na masomo bila ushauri wa wazazi wake, kwasasa tunataka aendelee na masomo.

Aidha, wachangiaji wengi walilalamikia utaratibu wa watoto waliofahulu vizuri na kupangiwa vyuo wakati wazazi hawana uwezo wa kulipa ada na kutaka asome kidato cha tano kwanza.

Juzi Katibu Mkuu Shemdoe alisema baada ya ufuatiliaji aligundua hali hiyo imetokana na kutokuwapo kwa mawasiliano sahihi baina ya mzazi na mwanafunzi juu ya michepuo waliyochagua

Alisema uchaguzi wa wanafunzi juu ya michepuo ulizingatia kuanzia chaguo la kwanza hadi la tano lililojazwa na mwanafunzi katika fomu maalum, pamoja na namna mwanafunzi alivyofaulu katika mchepuo husika.

"Hakuna ambaye amepangiwa asipochagua lakini tulichobaini ni mawasiliano duni baina ya wanafunzi na wazazi, kwamba mzazi anataka mwanae asome mchepuo huu na mtoto amejaza mchepuo mwingine sasa matokeo yanapokuja tofauti na waliyoongea mzazi ndiyo anaona mwanae ameonewa"alisema Profesa Shemdoe

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi, juu ya tahsusi ni wa kielektroniki, unaofanya uchaguzi na utambuzi na hupanga kulingana na ufaulu wa wanafunzi, hali inayoondoa uwezekano wa mwanafunzi kupangiwa tofauti na michepuo aliyoomba.



***Imenadikwa na Salome Kitomari (DAR) na Abdallah Khamis (MTWARA)***

# Lowassa, Mbowe walivyomlilia TB Joshua

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, wamemlilia Mhubiri maarufu wa kimataifa wa nchini Nigeria, Temitope Balogun Joshua maarufu jina T.B Joshua, aliyefariki dunia Jumamosi.

Lowassa alisema alikuwa ni kiongozi aliyeunganisha jamii bila kujali itikadi za kidini.

Amesema binafsi pamoja na Watanzania, wamempoteza rafiki wa kweli aliyependa Tanzania.

Lowassa aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, alipozungumza nan NIPASHE kuhusu kifo cha kiongozi huyo, kilichotokea juzi.

"Nimepokea taarifa za kifo cha rafiki yangu, TB Joshua kwa msthuko mkubwa sana. Hakika tumempoteza rafiki aliyekuwa na mahaba na Tanzania na Watanzania.

"Alikuwa si tu mhubiri lakini pia alikuwa ni kiongozi wa jamii ya watu wa imani zote. TB Joshua alikuwa ni mtu mwenye kutaka kuona jamii inaishi kwa amani na upendo," alisema Lowassa;

Mwenyezi Mungu ampokee katika ufalme wake. 'Rest In Peace' (Apumzike kwa Amani)."

**FREEMAN MBOWE**

Naye, Mbowe, kwenye ukurasa wake wa Twitter alisema kwamba, amepokea taarifa za kifo cha TB Joshua kwa mshtuko akisema alikuwa rafiki kiongozi wake wa kiroho.

"Nilishtuka na kusikitishwa na kumpoteza rafiki yangu, na mlezi wa kiroho, Nabii TB Joshua. Alinikaribisha katika SCOAN yake ya Lagos na aliniombea kwa faragha kwa ajili yangu na Tanzania, nchi ambayo aliipenda!

"Hakika, imeondoka mapema sana! RIP ndugu yangu. Kaka yangu TB Joshua," alisema Mbowe.

Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Dk. Benson Bana, akizungumza na Amka na BBC, kwenye Idhaa ya Kiswahili, jana, alisema taarifa ya kifo cha TB Joshua kimepokelewa kwa simanzi kubwa hususan kwa wafuasi wake, Nigeria.

"Kimepokelewa kwa hali ya sintofahamu kwa viongozi wa karibu waliomfahamu, kwa ujumla waumini wake, wafuasi wake wamekwenda kwenye kanisa lake jijini Lagos, wakiwa na simanzi kubwa.

"Wengine wakitaka waone mwili wake, wengine wakisema amesinzia atarudi tena, wengine walienda pale kwa matibabu, maombezi, mahubiri, lakini walivyofika asubuhi wanaambiwa TB Joshua hatunaye kwa kweli imewasikitisha," alisema Dk. Bana.

Alisema chanzo cha kifo chake kwa mujibu wa kamishna wa polisi Lagos hakijaelezwa , mwili wa TB Joshua ulipokelewa hospitalini saa 9 alfajiri, usiku wa kuamkia jana, na akatangaza kifo hicho rasmi jana.

"Hakuna kilichoelezwa kilichosababisha kifo chake, takwimu zinaonyesha kwamba siku mbili zilizopita alikuwa hajisikii vizuri.

"Hali yake haikuwa hali ya kuleta mashaka na sintofahamu mpaka siku ya Jumamosi alikwenda kanisani na kuwaasa waumini wake watenge muda vizuri wa kumuabudu Mungu, kurejea nyumbani kwa muumba wao.

"Tunaamini taarifa zitatolewa kwa sababu ni M-Yoruba na taratibu za kimila za kabila hilo, taarifa lazima zitolewe kwa kiongozi wa kimila na mpaka hivi sasa ninavyoongea (jana asubuhi) wafuasi wake walikuwa wanakwenda kwenye kijiji alichozaliwa kutoa taarifa za kifo," alisema.

Dk. Bana alisema kutokana na uzoefu alionao kwa misiba ya baadhi ya viongozi au watu wa Nigeria, miili hukaa muda mrefu.

"Miezi, miwili hadi mitatu hukaa, misiba ya wakubwa hawa. Haijulikani mazishi lini, ila kiongozi wa kimila amewashauri wafuasi watulie wasiushike mwili wake, kwa heshima ya mtoto wao atazikwa kwa taratibu za kimila, tunasubiri taarifa,"alisema Dk. Bana.

**MKE TB JOSHUA**

Mke wa TB Joshua, Evelyn, ambaye pia ni mmoja wa wahubiri wakuu wa kanisa la SCOAN, ameelezea kushtushwa na kifo cha ghafla cha muwe wake.

"Kumpoteza mwenza sio jambo rahisi; iwe ghafla ua la, inavunja moyo. Majonzi huharibu ustawi wetu kwa ujumla. Lakini cha msingi ni kumtumainia Mungu," alisema mke wa TB Joshua aliongeza kusema.

"Ni yeye tu (Mungu) anaweza kutufariji wakati huu mgumu."

## HABARI KITAIFA



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Raibu (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua duka la kusambaza vifaa vya umeme wa jua la D. Light, katika jengo la Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro (KNCU), katika manispaa hiyo, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. Wengine ni Ofisa Uendeshaji Mkuu wa D. Light Africa Jacob Okoth (kushoto), Mkurugenzi wa D. Light Charles Natai (wa pili kulia) na Mkuu wa Mauzo na Usambazaji D. Light Tanzania, Hamis Mruta. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yaihoji Jamhuri kuchelewa kesi ya Tundu Lissu

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imesema imefumbia macho muda mrefu kesi ya uchochezi inayomkabili, aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu na wenzake, imesimama siku nyingi haiendelei, hivyo upande wa Jamhuri umetakiwa kutoa maelezo.

Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, alisema hayo jana wakati kesi hiyo ikitajwa na upande wa Jamhuri kudai mshtakiwa Lissu bado yuko Ujerumani.

"Kesi imesimama muda mrefu, nimefumbia macho siku nyingi sana, Wakili wa Jamhuri hebu tuelezee,"alisema Hakimu Simba.

Akijibu Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanton, alidai shauri lilisimama sababu ya Lissu hayupo nchini.

Hakimu Simba alihoji kwamba kesi ya muda mrefu na vifungu vya sheria kadhaa vipo vinavyozungumzia mazingira kama hayo ambapo mshtakiwa anakuwa hayupo kwa muda mrefu.

Wakili Mitanto alidai kuna maombi ya wadhamini wa Lissu ya kujitoa kwenye udhamini endapo yatatolewa uamuzi yatatoa muongozo kwa upande wa kesi ya jinai.

Hakimu Simba alikubali hoja hizo na kuamuru kwamba pingamizi la Jamhuri lililowasilishwa kwenye maombi ya wadhamini litasikilizwa kisha uamuzi utatolewa ili kupata muongozo wa kesi ya jinai inayokwama kuendelea.

Mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi Julai 7 mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza pingamizi la Jamhuri kwenye maombi na kuitaja kesi ya jinai. Wadhamini wa Lissu waliomba kujiondoa kumdhamini mshtakiwa huyo na kuiomba mahakama iyatupilie mbali.

Miongoni mwa hoja katika pingamizi la upande wa Jamhuri ni kwamba Mahakama haiwezi kushughulikia jambo hilo na haina Mamlaka ya kusikiliza na kutolea uamuzi maombi hayo hivyo wanaomba yatupwe.

Katika kiapo kinzani Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo anadai Lissu aliruka dhamana tangu tarehe aliyopona na kuruhusiwa kutoka hospitali.

# Samia afuta hati 11 za mashamba

**Na Munir Shemweta,** KILOSA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefuta hati 11 za mashamba yenye ukubwa ekari 24,119, na kuagiza kugawiwa kwa wananchi wilayani Kilosa mkoani Morogoro, kwa ajili ya kilimo, ufugaji na uwekezaji.

Aidha, ameridhia ufufuaji wa mashamba 49 yenye ukubwa wa ekari 45,788.5 yaliyotaifishwa miaka ya nyuma, huku wananchi wakiwa hawana uhakika nayo, na kuagiza kutumiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo.

Uamuzi huo wa Rais Samia ulitangazwa jana wilayani Kilosa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, wakati akizungumza kwa nyakati tofati na viongozi, watendaji na wananchi wa kijiji cha Kimamba wilayani.

Alisema pamoja na kufutwa mashamba hayo haimaanishi kama yako huru kwa kila mtu kujichukulia bila utaratibu na timu maalum imeundwa kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi katika mashamba hayo na kutahadharisha asitokee mtu yeyote kuzuia timu hiyo kufanya kazi yake.

"Lazima tupange matumizi ya mashamba yaliyofutwa na utaratibu utaelekezwa na viongozi wa mkoa na wilaya na isitokee mtu kuja kujigawia mashamba na kila kipande cha ardhi kitapangwa na lazima ijulikane nani anamiliki," alisema Lukuvi.

Akielezea zaidi kuhusiana na mashamba 49 yenye ukubwa wa ekari 45,788.8 yaliyofufuliwa, Waziri Lukuvi alisema ekari 30,672.2 kati ya hizo lazima zirudi kwa wananchi na ekari 15,116.3 zilizobaki zipangiwe kwa ajili ya matumizi ya uwekezaji.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wananchi watakaopewa mashamba ni wale wasiokuwa na ardhi kabisa na asingependa ardhi itolewe kwa watu wenye nia ya kujilimbikizia maeneo na kusisitiza anachotaka ni mashamba yasaidie wale wananchi wa Kilosa kwa kujipatia kipato na kuinua maisha.

Naye, Mkuu wa mkoa wa Morogoro Martine Shighela, alimshukuru Rais kwa uamuzi wa kufuta na kufufua mashamba wilayani humo na kwamba itasaidia katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi.

Kwa mujibu wa Shigella, serikali hatasita kuchukua hatua kwa viongozi wa ngazi za vijiji watakaohusika kwa namna moja ama nyingine kuondoa utulivu wakati wa zoezi la kupanga matumizi ya mashamba yaliyofutwa.




Hadhi ya Mlima Kilimanjaro kurudishwa

# KINAPA: Tumedhamiria kurudisha uoto wa asili



Bwalo la kulia chakula katika Shule ya Sekondari Korikie, iliyoko Kitongoji cha Mamba, ni moja ya miradi iliyojengwa na KINAPA, kuhamasisha utunzaji wa mazingira ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. **PICHA: MTANDAO**

**Na Jenifer Gilla**

***Jana katika sehemu ya kwanza tulielezea jinsi majanga ya moto yanayoathiri Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, leo katika sehemu ya pili tunawaletea jinsi KINAPA ikishirikiana na wadau wengine wa hifadhi hiyo wanavyopambana kukabiliana na janga hili pamoja na mengine yanayosababisha kupungua kwa miti ya asili*.**

NI siku ya jumatatu asubuhi, anga imetawaliwa na ukungu, baridi ikipenya kwenye ngozi, lakini kwa namna ya aina yake ni hali hewa inayoleta raha inayojitegemea.

Hapo ndipo mbele yangu, nipo ana kwa ana na mwenyeji wangu, mzee Imani Kikoti, Ofisa Uhifadhi Mkuu anayesimamia Idara ya Sayansi na Uhifadhi katika mamlaka ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA). Sihitaji ushahidi kuthibitisha namna anavyohuzunika utajiri nakshi ya Mlima Kilimanjaro unavyosambaratishwa na mazingira.

Hapo ndipo ugeni wake wa Nipashe , ukapatwa na hisi ya kumdadisi nini mahususi kinamgusa?

Mzee Kikoti, anaianza sehemu yetu ya pili ya simulizi kwa kwa kauli ifuatayo;

"Zamani ilikuwa ukitoka hapo nje ya geti letu kwenye hicho kijiji na kutaka kitanda cha mbao inayotokana na mti wowote (mninga,mvule,mkongo), ilikuwa rahisi kupata, lakini sasa hali ni tofauti, vitanda hivyo havipatikani tena maeneo haya".

Ni maelezo ambayo yanabeba sehemu ya picha ya kilio cha kitaifa namna utajiri wa kimazingira na kiuchumi wa dunia uliobahatika kuwapo nchini ulihujumiwa, lakini kina mzee Kikoti na wadau wengine watetezi wa mlima huo wamefanikisha kudhibiti.

### WALIVYOSHTUKA

Mzee Kikoti anasimulia kwamba kwa uzoefu wa macho yao, mara moja walianza kuona uhusiano uliokuwapo kati kupungua kwa miti katika hifadhi hiyo na athari zinazoikumba.

Anasimulia, ushuhuda mwingine ukazidi kuwafungua macho, pasipo kuhitaji darasa la mazingira kwamba barafu ambazo miaka nenda rudi hazikuwa zikiyeyuka, sasa ni mithili ya friji ya barafu ambayo umeme wake umekatwa kwa muda mrefu.

"Mpaka hivi sasa theluji zimefikia kilometa za mraba 1.76, kikubwa ni ongezeko la joto ulimwenguni, kadiri siku zinavyoongeeka joto linaongezeka na barafu zinayeyuka" .

"Japokuwa mabadiliko ya tabia nchi yameuathiri mlima huu lakini kupungua kwa miti nako 'kumeongeza msumari kwenye kidonda' kwa sababu hakuna oksijeni ya kutosha kupambana na kaboni inayosababisha ongezeko la joto.

Ripoti Maalum ya Athari za Ongezeko la Joto kutoka jopo la Kisayansi la Umoja wa Mataifa la Kukabiliana na Mabadiliko ya Athari ya Hali ya Hewa (IPCC), inasema kuwa k joto limeongezeka kufikia 1.5°C na kama jitihada za haraka zakukabiliana nazo hazitofanyika linaweza kufikia 2°C.

Walistushwa pia na kutoonekana kwa baadhi ya wanyama na ndege waliozea kuwaona kwenye hifadhi hiyo.

"Kuna wanyama kama nyani ambao wanapenda kuwapo eneo lenye miti iliyokaribiana, yale maeneo ambao miti imekatwa kwa wingi wanyama hawa wamehama, kwa hivyo tusipofanya juhudi za kurudisha uoto asili katika hifadhi hii kuna hatari wanyama hawa wanaweza kutoweka kabisa", aliongeza.

Anarejelea kuwa wakati wavuna mbao wao wamezama kwenye utengezaji samani na wanawake kukata kuni kwa ajili ya kupikia, binadamu wengine wanasababisha mlima kuungua moto, ni wakala na watendaji wa hujuma za kijangili na wale wanaorina asali kwa siri ndani ya eneo la hifadhi lililopigwa marufuku ya shughuli za binadamu.

Mara hii akitumia lugha ya bashasha, tofauti na hisia zilizofungua mjadala na Nipashe, anasema wamefanikiwa kupunguza majanga ya moto yaliyokuwa yakitokea kila mara na sasa huchukua hata miaka 2 bila ya moto kitokea.

### WALIVYOJIDHATITI

Mwanamazingira Kikoti, katika wajibu wa mamlaka ya hifadhi Kilimanjaro kwa kushirikiana na wadau wamazingira, wapo katika kipindi endelevu cha kuzuia barafu kuendelea kuyeyuka milimani na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe inahamisha udadisi wake na kukinga sikio kupata ufafanuzi wa Theonest Kagwebe, Askari Mhifadhi Namba Moja anayesimamia Idara ya Ujirani Mwema ya KINAPA.

Kagwebe anasimulia aina ya urafiki na vijiji jirani unaofanywa na Mamlaka ya Hifadhi Mikumi kwa vijiji kama Kidogobasi kilichopo wilayani Kilosa, nao KINAPA wamejisogeza kwa jumla ya vijiji 92 vinavyouzunguka Mlima Kilimanjaro, ajenda yao kuu ikiwa ni elimu ya kina kuhusu mazingira na manufaa yanayohusiana nayo.

"Huwa tunazungukia shule zote zilizopo eneo linalozunguka hifadhi na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutunza mazingira katika hifadhi hii. "Pia, tunafanya mikutano kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji ili kutoa elimu kwa wanajiji.

"Kuna baadhi ya makosa tukiyakamata huwa hatumpeleki mtuhumiwa polisi bali tunampa elimu. Kwa mfano, ukimkuta mama kakata mti mdogo kwa ajili ya kupikia, kama ni kosa la kwanza huwa tunamuelimisha, akirudia ndio tutampeleka kituo cha polisi," anasimulia Askari Kagwebe

### KUDUMISHA UTAMADUNI

Kagwebe, akiwa katika ukomavu wake wa askari jamii , anataja staili nyingine ya kufanya kazi yao kudhibiti hujuma hizo za kimazingira, pia uhamasishaji wa jamii hizo kudumisha utamaduni wa kabila lao, ambalo kwa sehemu kubwa ni jamii ya wachagga.

Anaeleza: "Kupitia Idara ya Ujirani Mwema, tunatoa mbegu za mimea ya asili kama vile parachichi, kahawa na ndizi na kuhamasisha wanakijiji wapande kuzunguka nyumba zao, ikiwa ni utamaduni wao, pia kuongeza uoto asili".

Kiongozi huyo wa askari, anataja eneo lingine wanalowekeza ni urafiki na majirani hao kwa kusaidia miradi mbalimbali inayoombwa na wananchi, lengo ni kuwaonyesha faida inayopatikana kutokana hifadhi hiyo.

"Mpaka sasa miradi mikubwa ambayo tumeishaikamilisha ni ujenzi wa bwalo lakula chakula katika Shule ya Sekondari Korikie, iliyoko Kitongoji cha Mamba, Ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari ya Zakayo Mosha na ujenzi wa Zahanati ya Kitowo ambazo tumeshazikabidhi kwa Serikali" anasema.

### DORIA MASAA 24

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi anayesimamia idara ya Ulinzi na Uoakoaji, Mapinduzi Ndesa anasimulia kuwa wameona mafanikio kwa miaka 10 sasa, kwakuwa timu ya askari wa hifadhi hiyo wanafanya kazi usiku na mchana kwa kushirikiana na wanavijiji kuhakikisha wanakomesha ujangili unaoendelea.

"Kwa mwezi huwa tunakamata majangili wasiozidi 10, kutegemeana na msimu, mfano mwezi wa tatu tumekamata watu 10, kati ya hao 8 walikuwa wanawake waliokata kuni kwa ajili ya kupikia, hao wawili walikuwa wanakata magogo na umewapeleka kwenye vyombo vya sheria", anasema

Kauli hio inathibithishwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Msiri, Kata ya Marangu Mashariki, John Mtui, akitoa ushuhuda wa kijiji chake kushirikiana na KINAPA kudhibiti ujangili wa kibiashara.

"Mfano mwezi Aprili, mwaka huu tumekamata wanakijiji wa hapa kwetu wakiwa na kuni mbichi wakitokea msituni, tukawaripoti kwa mhifadhi kwa bahati mbaya wametoroka ila tunawasaka na tukiwapata tutawakabidhi kwa wahifadhi wa KINAPA," anasema mwenyekiti huyo.

Askari Ndesa anataja mbinu nyingine wanayoitumia kudhibiti uhalifu huo kuwa ni kunafanywa tahmini katika hifadhi hiyo kila, baada ya miezi mitatu kukagua kama kuna ukatwaji wa miti na inapogundulika kuwa kuna dalili ya kukatwa miti eneo fulani hapo kunafanyika doria kali.

***Je, wadau wengine wa vita vya kuitetea KINAPA na ustawi wake wana nafasi gani? Usikose makala inayofuata.***

HABARI KITAIFA

# Vipaumbele 13 vya uchumi vyaanikwa

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango imeanisha vipaumbele 13 vya kiuchumi ambavyo vinalenga kusaidia ukuaji wa uchumi kwa kuziba mianya ya upotevu, matumizi bora ya fedha na kulipa madeni.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Mwigulu Nchemba (pichani), aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo bajeti yake ni Sh. Trilioni 12.9.

Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 11.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 1. 025 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Alisema katika mwaka 2021/22, mafungu ya wizara ikiwamo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Muda wa Kati wa Mapato na Matumizi (MTEF).

Waziri Mwigulu alisema katika vipaumbele vya matumizi ya kawaida watafuatilia na kufanya tathmini, ukaguzi, udhibiti na uhakiki wa mapato, matumizi, miradi ya maendeleo, mali za umma na miamala ya utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Alisema wizara itafanya tathmini ya kina ya mfumo wa mapato na matumizi ya serikali ili kubaini maeneo yenye upungufu au matatizo na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua.

Alisema pia wataandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya PPP, kukamilisha maandalizi ya mwongozo wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na kufanya sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2022 na kutunga sera ya taifa ya idadi ya watu na mkakati wa utekelezaji wake.

Alisema katika mwaka 2021/22, mafungu ya wizara, ikiwamo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika MTEF.

Alifafanua kuwa katika vipaumbele vya matumizi ya kawaida, wizara inatarajia kufanya mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 - 2025/26) na kuanza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Waziri Mwigulu alitaja kingine ni kufanya tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali (DSA), kuratibu mipango na mikakati ya upatikanaji wa misaada, mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia bajeti ya serikali.



### MATUMIZI YA MAENDELEO

Waziri Mwigulu alisema wizara inatarajia kutekeleza mambo sita na kuyataja kuwa ni kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mikataba, ufuatiliaji na tathmini, usimamizi wa vihatarishi vya deni la serikali pamoja na vihatarishi vya ununuzi wa umma.

Alisema pia wataandaa mkakati wa kitaifa wa uchumi wa bahari, kuwajengea uwezo watumishi kutoka wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali, taasisi na mashirika ya umma, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za serikali.

Alisema wataimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za serikali na kuendelea na ujenzi wa jengo la wizara katika Mji wa Magufuli pamoja na jengo la Ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Geita.

### UDAHILI WANAFUNZI

Alisema katika vipaumbe vya kitaasisi wizara zinatarajia kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza tija katika uchumi na utoaji huduma.

Alisema taasisi za mafunzo na elimu ya juu zinatarajia kudahili wanafunzi 65,322, wakiwamo ngazi ya cheti 14,545, stashahada 17,735, shahada 31,602 na uzamili 1,440.

Alisema wanatarajia kuendeleza ujenzi wa vyuo kadhaa, kujenga nyumba za watumishi, mabweni uzio, vyumba vya madarasa, mgahawa na maktaba.

Alisema Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi katika ngazi anuai za usajili, kuendesha mitihani ya kitaaluma mara mbili kwa mwaka kwa watahiniwa 4,000 na kuendesha mafunzo endelevu yaani CPD 24 kwa wataalamu 3,000.

Alisema katika mwaka 2021/22, taasisi za rufani za kodi na ununuzi wa umma ambazo ni TRAB, TRAT na PPAA zitaendelea kupokea, kusajili, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufani za kodi na ununuzi.

Alisema Mamlaka ya Mosoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Bidhaa zitaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi, udhibiti na uendeshaji wa masoko hayo.

Kadhalika alisema wataandaa miongozo ya mazao yatakayouzwa sokoni kwa kushirikiana na wadau husika, kuongeza idadi ya mazao yatakayouzwa kupitia soko la bidhaa ambapo mazao hayo ni chai, mkonge, kakao, pamba, kahawa, na vitunguu.

Pia, alisema Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana inatarajia kufanya maboresho au kutunga sheria mpya ya udhibiti wa masoko ya mitaji na dhamana.

FSSP
Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION FOR A SECTOR MAPPING SPECIALIST**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide individual consultancy Services as a **Sector Mapping Specialist** to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The individual **Sector Mapping Specialist** will provide technical support and advice to Global Affairs Canada through identifying opportunities for clean technologies and trade in the inclusive growth sector in Tanzania.

Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:

i. Master's degree in relevant discipline, such as finance, economics or development, from a recognized University.
ii. Five (5) years of professional work experience in the international development sector in Tanzania.
iii. Five (5) years of professional experience in working with Development Partners.
iv. Five (5) years of professional work experience on inclusive growth and women's economic empowerment.
v. Previous experience conducting similar scoping studies, preferably in the areas of economic growth, inclusive growth and / or women's economic empowerment.
vi. Experience working with stakeholders from Non-Government Organizations and Government

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

i. Strong report writing and oral and visual presentation skills;
ii. Knowledge of national context for economic growth in Tanzania, including an understanding of relevant policies, priorities and programs of key institutions and development partners.
iii. Advanced professional proficiency in spoken and written English – level 4 and Kiswahili – level 4 as explained in http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng
iv. Knowledge of gender equality policy priorities and processes in Tanzania.

Interested individual candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **20th June 2021 at 23:59 hours.** Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

**JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DAR – ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NA. 08 YA 2020**

**PRIME PROPERTIES LTD .................................................. MDAI**
**HASNAIN GULAM HUSSEIN .................................................. MDAI**

**DHIDI YA**

**JANETH PETER ISHENGOMA.................................................. MDAIWA**
**MARK AUCTIONERS AND COURT BROKERS CO. LTD ................ MDAIWA**

KWA: 1. JANETH PETER ISHENGOMA
**DAR ES SALAAM.**

2. MARK AUCTIONEERS &COURT BROKERS CO. LTD
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake Mahakamani, ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya mdai ambayo yanapatikana katika Mahakama hii, mnahitajika kuhudhuria katika Mahakama tukufu nyinyi au wawakilishi wenu, ambao wanaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 11/06/2021 Saa Tano (05:00) Asubuhi kujibu madai yenu mbele ya **MH. E. B. Luvanda, J.** Munaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnatarajia kuvitumia katika utetezi wenu siku hiyo.

**ANGALIZO:** Usipohudhuria siku hiyo shauri litasikilizwa na kuamuliwa bila nyinyi kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe ...04.....mwezi wa ...June.... mwaka 2021.

**NAIBU MSAJILI**
**KANDA YA DAR- ES- SALAAM.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# PPP habari njema kwa Watanzania

**WIZARA** ya Fedha na Mipango, imekuja na programu ya ubia baina ya sekta ya Umma na sekta Binafsi (PPP), kwa lengo la kuwezesha ushirikiano kwa utaratibu wa ubia katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye uchukuzi, ujenzi, elimu, afya, mawasiliano, maji, michezo, viwanda na biashara.

PPP imekuwapo miaka mingi na kuna miradi ambayo ilitekelezwa kwa muundo huo, lakini haikuwa na mafanikio makubwa kutokana na kukosekana mazingira wezeshi yenye kuelekeza taratibu za kufuata katika kufanya maandalizi kabla ya kuingia mikataba.

Kutokana na hali hiyo, serikali iliandaa sera na sheria ya PPP ili kuwa na utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi kwa kutumia dhana hiyo.

Katika kufanikisha mabadiliko ya sasa kwa lengo la kutekeleza mpango huo kwa tija na ufanisi, kilichofanyika ni kuwa na timu ya watalaamu zilizoundwa kutoka taasisi mbalimbali za serikali kufanya uchambuzi wa miradi 41 kati yake imeandaliwa na kufanyiwa uchambuzi na Mamlaka za Serikali kutoka sekta mbalimbali na mradi mmoja umeandaliwa na mwekezaji kutoka sekta binafsi.

Hizi ni habari njema kwa Watanzania kwa tunaamini PPP ina mambo mengi mazuri kama kuongeza ajira, mapato, uzoefu, ubunifu na teknolojia, kwa kuwa hakuna ubishi kuwa asilimia kubwa ya ajira zinatokana na sekta binafsi.

Ni ukweli pia serikali zote duniani haziwezi kufanya biashara bali jukumu ni kuweka mazingira mbalimbali wezeshi.

Tunatarajia kuwa programu hiyo itakuja na mambo mazuri, ambayo yataonyesha tofauti ya zamani na sasa, kufukia mashimo yote yaliyojitokeza awali ikiwamo kuisababishia serikali hasara ilipokuwa inabinafsisha au kukodisha mashirika ya umma. Tinaamini pia kwamba hatua hii unatoa nafasi kwa Watanzania kunufaika.

Tunaamini sekta binafsi ikishirikishwa vyema tutaona ukuaji wake, ikiwamo kutoa mchango wake kwa maendeleo kwa taifa, ikiwamo kuongeza mzunguko wa fedha.

Pia, itasaida ukuaji wa teknolojia kwa manufaa ya taifa, ikiwamo kujifunza mambo mapya yanayotokea duniani, kwa maendeleo endelevu.

Tunatarajia kutakuwa na uwazi na ushirikishwaji ipasavyo kwa Watanzania ili kuomba kushiriki kwenye utekelezaji wa miradi hiyo, ambayo itakuwa na matokeo chanja kwa taifa.


Katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya mwaka 2021/22 imeweka vipaumbeele 13 huku kimojawapo kikiwa ni kuimarisha na kuboresha mfumo wa PPP kwa manufaa ya taifa.

Tuna hakika iwapo kutakuwa na usimamizi thabiti, ufuatiliaji, uwazi na uajibikaji kwa pande zote maana yake miradi yote itakayotekelezwa itakuwa na tija.

Nchi nyingi duniani zimepiga hatua kutokana na kuishirikisha sekta binafsi kikamilifu, na sasa ni wakati wa kuhakikisha inasonga mbele na kushika kasi ili kuona tofauti ya miradi inayotekelezwa na sekta binafsi na mingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii ikihamasishwa inaweza kuboresha miundombinu ya shule

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya matatizo yanayoikabili sekta ya elimu, ni uhaba wa madarasa na madawati katika shule za msingi na sekondari, hali inayosababisha baadhi ya wanafunzi kutoanza masomo kwa wakati na wengine kusomea chini ya miti.

Suala hilo la uhaba wa madarasa, si jambo la dharura, kwani limekuwa likitokeza kila mwaka na kuwa kama la kawaida na limezidi kupanuka mara baada ya Serikali kuanza kutoa elimu bure. Kila mwaka, baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari wanashindwa kuanza masomo kwa wakati kutokana na tatizo hilo, ambalo kwa namna moja au nyingine linaweza kuwa ndani ya uwezo wa jamii.

Kimsingi, shule za Serikali ni za umma wa Watanzania wa maeneo zilipo, ambao kwa umoja wao wanaweza kuzihudumia, badala ya kuwa na mtazamo kwamba, wao hawahusiki katika kuzihudumia.

Ninadhani, umefika wakati sasa kuelekeza nguvu katika kuhamasisha wananchi ili watambue umuhimu wa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya shule kwenye maeneo yao.

Kumekuwapo na mtazamo kwamba, shule ni mali ya serikali, ambapo baadhi ya watu hujiweka pembeni na kuacha kuzihudumia, na huenda hata uhaba wa madarasa na madawati kila mwaka ukasababishwa na mtazamo huo.

Kimsingi, Serikali inamiliki shule hizo kwa niaba ya wananchi (umma), kwani huduma zozote zinazotolewa na serikali zinatokana na kodi na michango mbalimbali inayopendekezwa na umma wenyewe.

Hivyo, shule inapokuwa na uhaba wa madarasa, madawati au ukosefu wa vyoo, umma hauna budi kuona matatizo hayo ni kujitahidi kuyatafutia ufumbuzi kadri inavyowezekana.

Wakati shule zikiendelea kukumbwa na uhaba wa madarasa, wapo baadhi ya wananchi ambao wamehamasishwa na kuwa mstari wa mbele kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo yao.

Kwa mfano, katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara, ujenzi wa sekondari za kata na vijiji unaendelea, lengo likiwa ni kuhakikisha hakuna watoto wanaosubiri ujenzi wa madarasa, au kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

Wakazi wa Kata ya Nyakatende ni miongoni mwa wale ambao wameamua kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa sekondari ya kijiji, ambayo ilianza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza Februari mwaka huu.

Kukamilika kwa shule, kumeifanya Kata ya Nyakatende kuwa na sekondari mbili, huku wananchi kata nyingine nao wakiendelea mkakati wa kuongeza sekondari mpya lakini pia kuongeza madarasa mapya katika shule za msingi.

Siri kubwa ya kufikia hatua hiyo, inaelezwa na mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney, kuwa kuhamasisha wananchi kutambua umuhimu wa kuhudumia shule za umma kwa vile ni zao. Kwa mujibu wa Dk. Anney, wilaya hiyo ina kata 21 na vijiji 68, na kwamba Serikali inashirikisha wananchi katika kuboresha miundombinu zake na kwamba mwitikio wa wananchi ni mkubwa.

Binafsi ninaamini kwamba, utaratibu kama huo ukifanywa na wananchi wa maeneo yote nchini, uhaba wa madarasa utakuwa historia, kwani kila shule itakuwa na madarasa ya kutosha.

Ujenzi wa sekondari za vijiji utasaidia kuwapunguzia wanafunzi kutembea mrefu unaosababisha wachelewe kufika shuleni kwa wakati, lakini pia kuepuka vishawishi vya njiani vinavyoweza kuwahabaribia malengo yao.

Inaelezwa kuwa mbali na fedha taslimu, nguvukazi ya wananchi wa wilaya hiyo imekuwa ikitumika kusomba, mawe, maji, mchanga na kokoto katika kufanikisha ujenzi wa madarasa mapya.

Kwa wananchi ambao bado wana mtazamo kwamba, shule hizo ni za serikali, waelimishwe na wahamasishwe kwa ajili ya kuzihudumia ili kuondokana na uhaba wa madarasa unaojitokeza kila mwaka.

Wanafunzi kusomea katika mazingira rafiki ni jambo la msingi ambalo linaweza kuchangia kuwasaidia kufanya vizuri kwenye masomo yao na hatimaye kutimiza ndoto zao za kielimu.

Hivyo ni vyema wadau wote wa elimu wakiwamo wazazi na walezi kushiriki uboreshaji wa miundombinu ya shule ili watoto wao wasome kwenye mazingira yatakayowawezesha kufanya vizuri katika masomo.

# Serikali yalipa deni la trilioni 6.84-/

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema imelipa deni lote lililoiva lenye thamani ya Sh. trilioni 6.84 ambapo kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni Sh. trilioni 4.10 na mtaji Sh. trilioni 2.68.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi Mwaka wa Fedha 2021/22, alisema deni la nje ni Sh. trilioni 2.74, ikijumuisha riba ya Sh. trilioni 0.63 na mtaji Sh. trilioni 2.11.

Alisema kazi nyingine zilizofanyika ili kudhibiti deni la serikali ni pamoja na kuhuisha mkakati wa muda wa kati wa usimamizi wa deni wenye lengo la kuendeleza soko la ndani la dhamana.

Pia, alisema kukamilisha mwongozo wa uandaaji wa miradi na utekelezaji wa Sheria ya mikopo, dhamana na misaada wa mwaka 2020 na kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni Novemba mwaka jana, ambayo imeonyesha kuwa, viashiria vya deni la serikali vipo ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Waziri Nchemba alisema katika kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, wizara imeendelea kuzingatia taratibu za kutoa, kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya serikali. Waziri Nchemba alisema serikali imeendelea kufanya uhakiki na kulipa madai mbalimbali ya watumishi, makandarasi, washauri elekezi pamoja na fidia kwa miradi ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na miradi ya maji.

Alisema katika mwaka 2020/21, washirika wa maendeleo waliahidi kuchangia katika bajeti ya serikali Sh. trilioni 2.8 na kati yake Sh. bilioni 949.32 ni misaada na Sh. bilioni 1,925.04 ni mikopo nafuu.

Alisema hadi Aprili, mwaka huu, washirika wa maendeleo wametoa Sh. trilioni 1.8, sawa na asilimia 70 ya makadirio ya kipindi hicho ya kuchangia Sh. trilioni 2.6.

Alisema kati ya kiasi hicho, misaada ya kibajeti ni Sh. bilioni 210.24, sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho, miradi ya maendeleo Sh. trilioni 1.4, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya Sh. trilioni 2.287 na mifuko ya kisekta Sh. bilioni 230.0, sawa na asilimia 87 ya makadirio ya Sh. bilioni 265.69 ya kipindi hicho.

Alisema katika mwaka 2020/21, wizara ilipanga kusimamia na kuratibu upatikanaji wa mikopo ya Sh. trilioni 4.9 kutoka katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti lakini hadi mwezi Aprili, mwaka huu, upatikanaji wake ni Sh. bilioni 3,992.71, sawa na asilimia 95.7 ya lengo la kokopa Sh. bilioni 4,170.01 katika kipindi hicho.



Wadau wa kampuni ya Assemble Insurance, wakiuliza maswali wakati wa uzinduzi wa huduma mpya ya Bima Bronze Jamii katika mkutano wa pamoja na wadau na mawakala wa bima nchini jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Bronze Jamii yaongeza ufanisi huduma za afya

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya Assemble Insurance, inayojihusisha na masuala ya bima imesema imekuja na huduma mpya ya Bima ya Bronze Jamii iliyozingatia ubunifu kwa lengo la kupanua huduma ya afya nchini.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mkuu wa kampuni hiyo, Dk. Emmanuel Bwana, jijini Dar es Salaam katika mkutano wa pamoja na wadau na mawakala wa bima nchini.

Dk. Bwana pia alieleza kuwa bima hiyo mpya imezingatia uhitaji wa kupanua huduma ya afya katika kufikia idadi kubwa ya wateja walio na uhitaji.

Assemble Insurance ambayo awali ilijulikana kama (AAR Insurance) ni miongoni mwa kampuni kubwa za Bima Afrika Mashariki na zinazofanya shughuli zake Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na Sudani Kusini kupitia washirika wake.

Alisema soko la bima ya afya kwa sasa linauhitaji wa huduma bora na za unafuu, hususani kwa watu wa kipato cha chini na cha kati, pia huduma hiyo ya Bronze Jamii itakidhi mahitaji ya soko huku ikiwa na mfumo rafiki na wa kueleweka kwa wateja wake.

"Bronze Jamii, inatoa huduma ya bima kwa familia, mtu binafsi na mashirika kwa bei nafuu kuanzia Sh. 360,000 hadi 450,000, huku mteja akipata huduma za matibabu kote nchini kupitia watoa huduma tiba, hospitali, kliniki, vituo vya utambuzi na maduka ya dawa," alisema.

"Tunaunga mkono juhudi za serikali kwa kuboresha huduma na kupanua upatikanaji wa huduma zetu kwa idadi kubwa ya watu nchini, pia tutaendelea kutoa huduma za kipekee na za nafuu kwa wateja wetu kwa kutoa suluhisho rahisi na la ushindani wa bima," aliongeza.

Alisema kuwa wana uzoefu wa huduma hiyu kwa zaidi ya miaka 35 na kampuni hiyo nchini ina ofisi zake, Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Zanzibar na Dodoma, ikiwa na zaidi ya wanachama 300,000, huku zaidi ya wanachama 40,000 wakiwa ni Watanzania.




# Sababu kasi ndogo ukuaji mikopo sekta binafsi hii

**Na Romana Mallya, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwingulu Nchemba, amesema kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imetokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, hususani utalii, usafirishaji na huduma za chakula na malazi.

Aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Waziri Nchemba alisema wizara kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kutumia nyenzo mbalimbali, ikiwamo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la jumla la fedha za kigeni, ili kudhibiti mfumuko wa bei pamoja na hali ya ukwasi katika soko.

Alisema pamoja na athari za ugonjwa wa corona, udhibiti thabiti wa ukwasi katika soko umewezesha ukuaji chanya wa mikopo kwa sekta binafsi kwa wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka unaoishia Aprili, mwaka huu, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20.

Alisema kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imetokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, hususani utalii, usafirishaji na huduma za chakula na malazi.

Alisema kutokana na usimamizi madhubuti wa sera za uchumi jumla, ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa na matokeo chanya ya wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka jana, ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2019.

Alisema kupungua kwa kasi ya ukuaji umetokana na athari za ugonjwa wa corona katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Waziri Nchemba alisema mwaka jana, sekta zilizokua kwa viwango vya juu ni pamoja: Sekta ya Ujenzi (asilimia 9.1); Habari na Mawasiliano (asilimia 8.4); Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 8.4); Huduma zinazohusiana na Utawala (asilimia 7.8); Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi (asilimia 7.3); Madini na Mawe (asilimia 6.7) na Afya na Huduma za Jamii (asilimia 6.5).

Alisema mwenendo wa viashiria vingine hadi Aprili ni mfumuko wa bei uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia 3.3, ikiwa ni chini ya lengo la asilimia tano (5); kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kwa nchi.

Alisema nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC); na nakisi ya bajeti inatarajiwa kutozidi asilimia 2.6 kutokana na mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya serikali.

# NaCoNGO yapewa siku 30 kufanya uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, Dk. Dorothy Gwajima ametoa siku 30 kufanyika uchaguzi wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya kiserikali (NaCoNGO), kutokana na uongozi kutofanya uchaguzi huo kwa mara tatu mfululizo.

Aidha, ameunda kamati ya mpito ya mashirika hayo yenye wajumbe 10 ili kufanikisha haraka uchaguzi huo kwa mujibu wa kanuni zilizopo.

Dk. Gwajima akitoa jana tamko la kamati hiyo kwa waandishi wa habari jijini hapa, alisema Wizara hiyo haitavumilia tena watendaji wa washirika ambao wanatekeleza wajibu wao kwa kasi ambayo hairidhishi kwa kuwa inaathiri utekelezaji wa majukumu ya serikali.

Alisema Desemba 3, mwaka 2019, Bodi ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali iliiagiza baraza hilo kufanya uchaguzi na kuwapa muda wa miezi nane hadi Novemba 30, mwaka jana agizo hilo halikutekelezwa.

"Pia Bodi iliwaongezea tena siku 14, kuanzia Machi 3 hadi 17 mwaka huu pia walishinwa kutekeleza maagizo na Bodi kipitia kikao chake cha 46 ilitoa siku 40 hadi Juni mosi mwaka huu baraza liwe limefanya uchaguzi lakini halijatekelezwa,"alisema.

Alisema kuitofanyika kwa uchaguzi huo ni uzembe. "Huu ni uzembe mubashara watu wameamua kutofanya miezi nane, wiki mbili tena miezi mingapi, ndio maana nikasema tufanye maamuzi haya, na Katibu Mkuu utaandaa taarifa ya watu wenye utekelezaji wa namna hii uwalete tuchukue maamuzi," alisema.

# Watumishi Chato wawekwa kikaangoni

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WATUMISHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato ambao hawakuhudhuria maadhimisho ya siku ya mazingira duniani kimkoa yaliyofanyika wilayani humo mkoani Gieta,wameagizwa kuripoti kwa Mkuu wa Wilaya ili kutoa maelezo kwa nini hawakushiriki.

Maadhimisho hayo kimkoa yalifanyika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Chato.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Wlaya. ya Bukombe, Said Nkumba, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Sitaki, aliyemwakilisha katika kilele cha maadhimisho hayo yaliyofanyika wilayani Chato.

Alitoa agizo hilo baada ya kubaini kwamba watumishi wengi wa halmashauri hiyo hawakushirki katika maadhimisho hayo. Nkumba alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halamshauri ya Wilaya ya Chato kuwabaini watumishi wote ambao hawakuhuria maadhimisho hayo kimkoa.

Alisema baada ya kuwabaini awapeleke kwa Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho, ili kujieleaza ni kwanini hawakuhudhuria wakati suala la mazingira ni la kitaifa. Akiwahutubia washirki katika maadhimisho hayo, Nkumba ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Geita, alisema suala la uhifadhi wa mazingira ni la muhimu na kila mmoja anatakiwa kuwajibika kwa nafasi yake.




Mfanyabiashra wa mafagio akitafuta wateja katika eneo la Ilala Boma jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI NA 50 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**DR. SERVACUS BEDA LIKWELILE**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**RAYMOND BABU LIKWELILE**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24th mwezi JUNE 2021

Imewasilishwa leo Dar Es Salaam leo tarehe 26th mwezi MAY 2021

NAIBU MSAJILI

**KUPOTEA KWA CHETI**



**MTABUZI LINKOLINI KILONGOZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4142-0115** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ST.SOSTHENES mwaka 2014.yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/683811/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha SINZA mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi na 146 /2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**

**EDWIN JEREMIAH LYIMO WA SINZA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LEAH MESHAKI LAIZER**

**TANGAZO**

**(kanuni 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 30 mwezi 6 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye wosia anaweza kuuleta mahakamani.
Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 6 mwaka 2021

**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI.**

**ELIADAN IDRISA KADORY** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJI** aina ya **TVS KING** yenye namba za usajili **MC 289 CHS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/285949/2021.**

## DC: Viwanda viipe ushirikiano OSHA

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Filbert Sanga, ametoa wito kwa wamiliki wa maeneo ya kazi hususan viwanda kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ili mamlaka hiyo iweze kuwaongoza katika kuboresha mazingira yao ya kazi.

Sanga aliyasema hayo alipotembelewa na Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, ambaye alifanya ziara katika Kiwanda cha Fujian Hexingwang, kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya kuboresha mifumo ya usalama na afya katika kiwanda hicho yaliyotolewa awali na wataalam kutoka OSHA.

"Nawashukuru OSHA kutembelea kiwanda chetu cha Fujian Hexingwang kinachozalisha nondo na kuchukua hatua kufuatia ajali iliyotokea mwezi uliopita. Naomba ziara hizi ziendelee pia kwenye viwanda vyote vilivyopo wilayani kwetu ili kuhakikisha kwamba wamiliki wa viwanda wanafuata na kutekeleza maelekezo yote yanayohusu uboreshaji wa usalama na afya kwa wafanyakazi," alisema Sanga.

Naye Mwenda, akizungumza baada ya kukagua maboresho yaliyofanyika katika kiwanda hicho, alisema taasisi yake imeridhishwa na maboresho ya awali yaliyofanyika na hivyo kuondoa hati ya zuio la kufanya uzalishaji iliyotolewa hapo awali ambapo wametoa hati ya maboresho.

## Kasi ya upimaji wa rdhi yapaa

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Arusha imesema meongeza kasi ya upimaji ardhi katika maeneo mbalimbali katika kipindi cha mwaka mmoja toka kuanzishwa ofisi hiyo.

Hayo yalibainishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Arusha, Leo Komba, wakati akizungumzia mafanikio ya mwaka mmoja tangu kuanza rasmi kazi kwa ofisi yake mwezi Mei 2020.

Alisema, ongezeo hilo la upimaji ardhi limetokana na kasi kubwa ya upimaji ardhi inayofanywa na ofisi yake kwa kushirikiana na ofisi za ardhi kwenye halmashauri za wilaya na miji za mkoa huo ambapo takwimu zake zinaonesha ongezeko hilo ni mara mbili ukilinganisha na mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa Komba, wakati ofisi yake ilipozinduliwa upimaji ardhi kwa mkoa mzima ulikuwa viwanja 41,000, lakini hadi kufikia Mei 2021 mkoa huo umepima viwanja 81,215 ikiwa ni mara mbili ya viwanja vilivyopimwa kabla ya kuanzishwa ofisi hiyo ambapo kati ya viwanja hivyo 33,057 ni vya urasimishaji makazi holela.

"Baada ya ongezeko hilo la upimaji kasi ya uandaaji hati nayo imeongezeka ambapo kazi iliyopo mbele yetu ni kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchukua hati za ardhi kwa kuwa mwananchi atakapopata hati atakuwa ameongeza thamani ya ardhi yake" alisema Komba.

Akielezea ukusanyaji kodi ya Pango la Ardhi katika Mkoa wa Arusha, alisema mapato ya kodi hiyo yameongezeka kwa asilimia 30 ukilinganishwa na mwaka jana katika kipindi cha mwezi wa tano ambapo ofisi yake ilikusanya Sh. bilioni 5, lakini hadi sasa ofisi hiyo inakimbilia Sh. ilioni 8 na ni matarajio kufikia Juni 30, 2021 watakuwa wamefikia bilioni 8.9.

Kuhusu kero za ardhi, Komba alisema kasi ya kutatua kero za wananchi kuhusiana na masuala ya sekta ya ardhi kwa sasa imekuwa rahisi kwa kuwa ofisi hiyo inaweza kufanya ziara za kushtukiza kwenye maeneo mbalimbali.

# Bosi TMDA akemea vitendo vya rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI Mkuu Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA), Adam Fimbo, amesema Mamlaka hiyo haiko tayari kumvumilia mkaguzi atakayebainika kujihusisha na rushwa, sheria itafuata mkondo wake.

Fimbo aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wakaguzi wapya wa dawa na vifaa tiba yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.

Alisema mkaguzi hapaswi kujihusisha na rushwa ili kulinda taswira ya nchi na taasisi hivyo ni jukumu la kila mmoja kusimama kwenye nafasi yake na kuachana na vishawishi vitakavyomsababisha kuangukia kwenye rushwa.

"Wafanyabiashara hasa wa dawa wanapenda wakati mwingine kuwashawishi kuchukua rushwa... nendeni mkafanye kazi msile rushwa, tumeweka utamaduni wa kutokula rushwa... suala hili kwetu ni mwiko, na hatutamvumilia yeyote atakayeingia huko," alisisitiza.

Aliwataka wakaguzi hao kuzingatia kukagua, kudhibiti na kutoa elimu kwa umma ili kusiwapo na dawa feki zinazoingia sokoni.



Wafanyakazi wa mgodi wa Barrick wa Buzwagi wakishiriki zoezi la kupanda miti ya miembe katika maeneo ya mgodi wakati wamaadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watumishi wanolewa madhara ya vipodozi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATUMISHI wa umma katika taasisi mbalimbali mkoani Ruvuma wameanza kupata elimu kuhusu madhara ya matumizi ya vipodozi vyenye viambata vya sumu kiafya, hatua itakayowawezesha kuwa mabalozi wazuri ndani ya jamii na familia zao kwa ujumla.

Elimu hayo yalianza kutolewa kuanzia Mei 31, mwaka huu ikilenga taasisi saba za umma ikiwa ni mwendeleza wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutoa elimu kwa umma kuhusiana na madhara ya vipodozi vyenye viambata vya sumu.

Meneja wa TBS Kanda ya Kusini, Amina Yasini, alisema wameona watoe elimu kwa watumishi wa umma kwa sababu wanatambua kwamba muda mwingi wanakuwa na majukumu mengi, hivyo inawezekana hawasikilizi vipindi vya redio au kuingia kwenye mitandao ya kijami kupata elimu ambayo imekuwa ikitolewa na shirika hilo.

"Kwa hiyo tumeona tukitoa elimu kwa watumishi wa umma ana kwa ana inaweza kuwasaidia moja kwa moja hadi kwenye familia zao na majirani kuhusu madhara ya vipodozi vyenye viambata vya sumu," alisema.

Alisema moja ya majukumu ya TBS ni kudhibiti vipodozi ambavyo vina viambata vya sumu lengo likiwa ni kulinda afya za watumiaji.

Alifafanua kwamba Tanzania imepakana na nchi nyingi, ambako kuna mipaka mingi iliyo rasmi na isiyo rasmi, hivyo bidhaa nyingi zinaingia nchini. "Kwa hiyo shirika letu lina jukumu la kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia nchini ni salama kwa matumizi ya binadamu," alisema Yasini na kuongeza;

"Tuna utaratibu wa kupita kwenye masoko kuangalia bidhaa na tukikuta bidhaa ambazo tuna mashaka nazo tunazipima na tukibaini zina viambata sumu tunazikamata na kuziondoa sokoni."

Katika Mkoa wa Ruvuma maofisa hao wa TBS wanatarajia kutoa elimu kwa mashirika takribani saba ambapo sasa wanaendelea kutoa elimu katika Wilaya za Madaba, Mbinga na Nyasa.

# Serikal: Marufuku kufufukuza mwanafunzi kisa michango

SERIKALI imepiga marufuku kumfukuza mwanafunzi shule kwa sababu ya michango.

Aidha, imesema uchangiaji katika elimu unaoruhusiwa ni wa hiari na hauhusishi wanafunzi kuzuiwa kuhudhuria masomo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akiongezea majibu ya nyongeza katika swali la nyongeza la Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenani.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema wananchi wamekuwa wana mwitikio hafifu wa kuchangia kutokana na kudhani kuwa elimu ni bure kama ilivyotamkwa.

"Mheshimiwa Waziri yupo tayari kulieleza bunge na wananchi wakajua kwamba kilichobadilika ni elimu bila ada na utaratibu wa michango umebadilishwa kwa kwenda kuomba kibali lakini wanapaswa kuchangia maendeleo,"alisema.

Prof. Ndalichako akijibu swali hilo, alisema utekelezaji wa waraka namba tatu wa mwaka 2016 unaelezea utaratibu wa kutoa michango shuleni.

Alitoa wito kwa wazazi kushirikiana na serikali kuboresha mazingira ya shule uanapokuwa mazuri watoto wanakuwa na uhakika wa kupata elimu bora.

Awali, akijibu, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema Waraka namba tano wa elimu wa mwaka 2015, unazungumza kuwa elimu bila ada, na kuna waraka mwingine unaoeleza wajibu wa wananchi.

"Tunaendeleza kufanya tathmini kila wakati na kuboresha,nchi zima kwasasa tuna watoto milioni 14 kwa hiyo lazima serikali tufanye tathmini ili kuangalia jinsi ya kusaidia sera ya elimu kwa ujumla,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji ni kwa nini wazazi wanachangishwa michango ya kuchangia elimu wakati serikali inasema elimu ya Shule ya msingi na sekondari ni bure.

Akijibu, Naibu Waziri Silinde alisema serikali kupitia Waraka wa elimu namba tano wa mwaka 2015 iliamua kutoa elimumsingi bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne.

"Uamuzi huo ulijielekeza katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wenye rika la elimumsingi wanapata elimu bila kikwazo chochote ikiwemo ada au michango,"alisema.

Aidha, alisema serikali ilitoa Waraka wa elimu namba tatu wa mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila malipo.

"Waraka huu unafafanua maana ya elimumsingi na kuainisha majukumu ya kila kundi linalohusika katika utoaji wa elimumsingi bila malipo na kuweka utaratibu wa utekelezaji wake," alisema.

Aidha, alisema majukumu ya jamii na wananchi kuhusu michango yamebainishwa kwenye Waraka wa elimu namba tatu.

"Waraka unaeleza kuwa Kamati za Shule au Bodi za Shule zitashirikisha jamii katika maazimio na maamuzi ya masuala mbalimbali yanayohusu maslahi na maendeleo ya shule hususan uchangiaji wa hiari na kuwasilisha maamuzi hayo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili kupata kibali,"alisema.



Naibu Spika, Dk.Tulia Ackson (wa pili kulia), akiwa na baadhi ya wabunge wa Bunge la Malawi pamoja na maofisa wa Bunge hilo, wakiwa kwenye eneo la wageni mashuhuri la Bunge jijini Dodoma jana. Wabunge hao wapo nchini kwa ziara ya kulitembelea Bunge la Tanzania. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Timu yawasilisha taarifa kuhusu migogoro ya mipaka

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema timu iliyoundwa kwa ajili migogoro ya mipaka kati ya vijiji vya Mwanholo na Nyenze dhidi ya mwekezaji na mchimbaji madini Eli Hilal wilayani Kishapu imewasilisha taarifa yake na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk.Festo Dugange aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kishapu (CCM), Boniphace Butondo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itatua lini migogoro huo.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange, alisema Ofisi hiyo ya Mkuu wa Mkoa inaendelea kufanyia kazi taarifa iliyowasilishwa ili kubaini masuala yanayoweza kushughulikiwa na Mkoa na yale yanayohitaji uamuzi wa ngazi za juu.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inatambua mgogoro huo unaohusisha eneo lenye ukubwa wa hekta 2,872.4.

Alisema eneo hilo awali lilikuwa linamilikiwa na mgodi wa Wiliamson Diamond Ltd na kabla ya kugawiwa kwa mchimbaji Eli Hilal ambaye alimilikishwa na serikali.

"Baadhi ya wanakijiji wa Mwanholo na Nyanze hawaitambui mipaka ya eneo la mwekezaji wa uchimbaji wa madini na wengine wanalalamikia maeneo yao kutwaliwa na Mwekezaji wa uchimbaji bila kulipa fidia," alisema.

Dk. Dugange alisema mwezi Februari 2021 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga iliunda timu ya wataalamu kwa ajili kufanya uchunguzi wa mgogoro huo.

"Timu iliyoundwa imewasilisha taarifa yake na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga inaendelea kufanyia kazi taarifa iliyowasilishwa ili kubaini masuala yanayoweza kushughulikiwa na Mkoa na yale yanayohitaji uamuzi wa ngazi za juu,"alisema.

Alisema serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga itashirikiana na wananchi na wadau wote muhimu katika kutatua mgogoro huu na kuhakikisha haki inatendeka.

## Maandalizi yaendelea mradi wa miundombinu

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inaendelea na maandalizi ya Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Mijini (TACTIC) na Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam Awamu ya II (DMDP II) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara, madaraja, stendi za mabasi na masoko.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde,aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwaongezea Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hasa ikizingatiwa ukuaji wa kasi wa Miji na Halmashauri.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imeitengea TARURA Sh.Bilioni 400 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja.

"Bajeti hiyo ni ongezeko la Sh.Bilioni 124.97 kutoka bajeti ya Sh.Bilioni 275.03 iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2020/21,"alisema.

Alisema sambamba na kupatia TARURA fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika miji inayokua kupitia mipango mbalimbali.

"Kama vile Mpango wa Uboreshaji wa Miji Mikakati ambayo ilihusisha Majiji na Manispaa kupitia Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (TSCP), Programu ya Kuimarisha Halmashauri za Miji 18 (ULGSP) ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP)," alisema.





**Habari zote na Augusta Njoji**

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Juni 8, 2021



Ukurasa 12

‘Kilichoua Ushirika ni hiki, mikakati kuuinua yatajwa’



Ukurasa 14

Kiswahili Pwani VS Maziwa Makuu

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# COVID-19 inavyozidi kuumiza waathirika wa udhalilishwaji



Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Vuga Unguja, Valentina Ketema (wa kwanza kulia), akizungumza katika Mkutano wa Wadau wa Masuala ya Udhalilishaji, uliofanyika katika ofisi za TAMWA Zanzibar.**PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

JANGA la corona linaloelezwa kuwa limeleta athari na taharuki karibu dunia nzima, unaweza usidhani kuwa linaweza kuwa chanzo cha kukwamisha kesi kortini.

Hilo limetokea visiwani Zanzibar, ugonjwa huo umeathiri mwenendo wa mahakama kwa kukwamisha kupatikana ushahidi.

Licha ya shughuli za kijamii na kiuchumi kuendelea baada ya kasi ya corona kupungua athari zilizotokana na ugonjwa huo zimesababisha ukosefu wa nauli kwa mashahidi wa kesi za jinai, zikiwamo za udhalilishaji wanawake na watoto.

Kwa mujibu wa taratibu za kisheria mashahidi wa kesi za jinai hugharamiwa nauli za kwenda kortini na kurudi makwao, kila wanapohitajika mahakamani, anasema Hakimu dhamana wa mkoa wa Kusini Unguja, Khamis Ali Simai.

Anaeleza kwamba corona imesababisha ukosefu wa fedha za kusafirisha mashahidi tangu ilipozuka mwanzoni mwa mwaka jana.

“Imepelekea mashahidi kujigharimia nauli na hili ni tatizo kwa vile wengine hawana uwezo,” Anasema Simai.

Anataja sababu ya mashahidi kukosa fedha hizo kuwa ni bajeti finyu inayotolewa na serikali kwa mahakama kutokana na corona kusababisha kutetereka kwa uchumi.

Hakimu huyo anaeleza kuwa kabla ya kuzuka ugonjwa huo mashahidi walilipwa nauli ili kuhudhuria mahakamani lakini sasa inakuwa vigumu.

Anawataka mashahidi hasa wa kesi za udhalilishaji, kutovunjika moyo wafike mahakamani kutoa ushahidi kwa vile bila ya uwepo wao inakuwa vigumu washtakiwa kutiwa hatiani.

**KITISHO UDHALILISHAJI**

Ofisi ya Takwimu ya Serikali Zanzibar inasema matukio ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyokusanywa na taasisi mbalimbali pamoja na Jeshi la Polisi, mwaka jana ni 1,363.

Inasema waathirika wa matukio hayo ni wanawake 217 ambayo ni asilimia 15.9, watoto 1,146 sawa na asilimia 84.1 na miongoni mwao wasichana ni 899 ikiwa ni asilimia 78.4 na wavulana ni asilimia 21.6 waathirika wakifikia 247.

Katika matukio hayo kesi 544 zinaendelea kusikilizwa mahakamani huku 382 zikifanyiwa upepelezi nyingine 197 zipo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka wakati 110 zimefungwa kutokana na sababu mbalimbali.

Katika matukio haya watuhumiwa 65 wametiwa hatiani wakati 25 wamefungwa na saba wameachiwa huru kutokana na sababu mbalimbali hasa kukosekana ushahidi.

**WASHTAKIWA KUNUSURIKA**

Sabra Ali, Ofisa Jinsia wa Wilaya ya Magharibi A, anasema kesi nyingi za udhalilishaji hufutwa kwa sababu kadhaa ikiwamo washtakiwa kutotiwa hatiani kutokana na kukosekana ushahidi.

“Mashahidi kushindwa kufika mahakamani pengine kwa kukosa nauli ni sababu mojawapo lakini muhali (kuoneana aibu) pia huchangia kwa kuwa wahusika na mashahidi hawatokei mahakamani.”

Anaeleza kuwa wengi wa wahanga wa udhalilishaji ni wanyonge ambao hawana uwezo wa kuwapa nauli mashahidi na huduma nyingine za kuwafikisha kortini.

Wakati mwingine mashahidi huitwa mara kadhaa na wakati wote hawafiki.

Anaitaka mahakama kuandaa mfuko maalum wa kuisaidia jamii ili kuwapo na wepesi wa watu kwenda kutoa ushahidi mahakamani wanapohitajika bila hivyo.

**WAATHIRIKA WALALAMIKA**

Mzazi wa mtoto aliyelawitiwa (jina tunalo), anasema kesi yake ipo mahakamani na alishawasilisha majina ya mashahidi kwa gharama zake na sasa anasubiri hukumu.

Anasema alitakiwa kuwasilisha mashahidi watatu na alilazimika kuwagharamia kwa kuwapa nauli ya kwenda na kurudi muda wote.

“Kama ningekuwa sina fedha mashahidi wangeshindwa kufika mahakamani maana waliniambia wanataka kutoa ushahidi, lakini hawakuwa na nauli”, anaeleza.

Anaiomba serikali kufanya juhudi za kuwawezesha mashahidi kufika mahakamani kwani bila wao hakuna kesi.

**MAONI YA WANAHARAKATI**

Mwanaharakati wa mtandao kupinga vitendo vya udhalilishaji wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hadia Ali Makame, anasema baadhi ya mashahidi hata wanapopewa nauli hukataa kufika mahakamani kutoa ushahidi.

Anasema ni vizuri kutilia maanani kwamba shahidi unapoitwa kwenda mahakamani hulazimika kuvunja baadhi ya shughuli zake kwa siku hiyo, ikiwa pamoja na kujipatia kipato. Kwa hivyo ni vyema serikali kurejesha utaratibu wa kulipa nauli.

Anaeleza kuwa hivi sasa mashahidi wanajigharamia wenyewe kufika mahakamani na baadhi yao wanakaa mbali na kulazimika kutumia zaidi ya Sh. 3,000 kwa nauli.

“Kwa wakazi wa vijijini, wengi wao ni wanyonge, kuitoa Sh. 3,000 kumwezesha kwenda na kurudi mahakamani ni shida”, anasema.

Time Asaa, kutoka Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), anasema ni vizuri kwa mashahidi na hasa wa kesi za udhalilishaji kupewa fedha ya nauli ili kutoa ushahidi mahakamani na haki ipatikane.

Anaeleza kuwa mbali na pesa ya kufika mahakamani ni vyema kutazama uwezekano wa pia kuwapatia fedha japo kidogo za kujikimu kwa siku nzima anayofika mahakamani.

Anasema shahidi unapomwita mahakamani unamvunjia shughuli zake za kujitafutia kipato, lakini ukimpa posho ya kujikimu hatakuwa na muhali wa kufika mahakamani.

Kwa ujumla tatizo la mashahidi kutofika mahakamani na kusababisha kesi nyingi za udhalilishaji kukwama au kufutwa zinafaa kumulikwa na hatimaye kupatikana ufumbuzi.

Hapo ndipo tatizo la mashahidi kuchangia haki kutoonekana kutendeka .

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# Kilichoua Ushirika hiki hapa, mikakati ya kuinua yatajwa



JULAI 3, mwaka huu ni siku ya Maadhimisho ya Ushirika Duniani na kwa Tanzania inaadhimishwa wakati taifa likiwa na vyama vya ushirika 8,040, vyenye wanachama takribani milioni 1.4.

Mwaka huu maadhimisho hayo yanafanyika mkoani Tabora kwenye viwanja vya Nane Nane, na yanatarajiwa kuvuta hisia za wanaushirika wengi zaidi, anasema Katibu Mtendaji wa Shirikisho la vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), Florian Haule(pichani).

Anaeleza TFC ilivyojipanga kuinua sekta hiyo ambayo kwa sasa imeonekana kushuka kutokana na changamoto mbalimbali.

Haule anasema zipo sababu nyingi ambazo zimepelekea ushirika kushuka hapa nchini tangu kufanyika maadhimisho ya kwanza miaka 20 iliyopita.

Katibu Mtendaji wa TFC, anaweka wazi sababu za kuporomoka na kwamba shirikisho limejipanga kuhakikisha ushirika unarudi katika kasi yake kama ilivyo miaka ya nyuma wakati ukianzishwa.

"Lazima tuwe wakweli ushirika umepitia changamoto nyingi, lakini tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa umepita mabonde na milima ingawa tunapambana ili usimame na dalili njema tumeanza kuziona," anasema.

Anaeleza kuwa sababu za kuanguka kwa ushirika ni nyingi lakini pia wizi kwenye vyama vya ushirika ni sababu moja wapo kubwa.

**JINSI UNAVYOKWAMA**

Haule anaeleza sababu za kuanguka kwa ushirika nchini, akisema ni pamoja na ukosefu wa weledi kwa baadhi ya viongozi ambao watu wengi waliona ushirika ni sawa na genge la wezi au eneo la kupora na kujitajirisha.

"Huku nyuma ushirika ulikuwa na nguvu sana na ndiyo maana ilifika sehemu ushirika ulikuwa unajiendesha kwa mali zake nyingi, kuanzia majengo, magari, rasilimali na vitega uchumi vingine kama vyuo na shule, lakini baadae serikali ilichukua baadhi ya mali za ushirika.

Lakini, kwa mujibu wa Haule, pia baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kutokuwa waaminifu na kutumia ovyo fedha za vyama vya ushirika ni moja ya jambo lililoviangusha.

Hilo lilipelekea watu kuanza kuwa na mashaka na kujitoa na huo ukawa ndiyo mwanzo wa kuanguka kwa ushirika japo vyama vya ushirika bado vipo katika maeneo mbalimbali hapa nchini, anasema Haule.

Anaeleza kuwa moja ya sababu ya kutaka kuiomba serikali kurejesha kwa ushirika baadhi ya mali kama vile majengo ni kujaribu kuinua tena uwezo na kujijenga zaidi.

Anasema pia kuna haja kwa serikali kuweka mkazo sera za ushirika na kuziweka katika mpango mkakati wa maendeleo na ikiwezekana kuingizwa kwenye bajeti.

"Lakini pia kuna haja ya kutoa elimu ya ushirika kwa viongozi na watunga sera kwa kuwa taratibu za ushirika haziingiliwi na taasisi nyingine kwa kuwa ushirika ni muungano wa hiari na wenye uamuzi wa nini cha kufanyika kwenye ushirika huo ni wenyewe wana ushirika na sio kuingiliwa na viongozi wa siasa," anasema Haule.

Anawataka Watanzania wajiandae kwa maadhimisho hayo ya mwaka huu ambayo pamoja na shughuli mbalimbali za vyama vya ushirika, kuna kazi za kijamii kwa wanaushirika.

"Kutakuwa na elimu ya utunzaji wa mazingira pamoja na kupanda miti, lakini pia kwenye maadhimisho hayo wanaushirika watachangia damu kwa ajili ya wenye mahitaji," anasema Haule.

**WATEGEMEEE NINI?**

Haule, anasema kuelekea kwenye maadhimisho ya mwaka huu yatakayoanza Juni 29 mpaka Julai 3 mkoani Tabora, ujumbe wao kwa serikali unabakia kile walichokiomba kwenye maadhimisho ya mwaka 2018.

> "Lakini pia kuna haja ya kutoa elimu ya ushirika kwa viongozi na watunga sera kwa kuwa taratibu za ushirika haziingiliwi na taasisi nyingine kwa kuwa ushirika ni muungano wa hiari na wenye uamuzi wa nini cha kufanyika kwenye ushirika huo ni wenyewe wana ushirika na sio kuingiliwa na viongozi wa siasa," anasema Haule.

" 2018 mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Kassim Majaliwa, tulimpa kilio kuomba serikali iturejeshee zilikuwa mali za ushirika ili zirudi kwetu," anasema Haule.

Aidha, mwaka huu wamepanga kuikumbusha tena serikali kuona umuhimu wa ushirika kuwa na mali zake na hii itakuwa chachu ya kuupeleka juu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Katibu Mtendaji huyo anasema kuwa watu wengi hawajui maana ya ushirika na ulianzia wapi na kufafanua kuwa ni muungano wa hiari wa jamii fulani, walioamua kuungana kwa pamoja ili kutatua matatizo yao ya kijamii kiuchumi na kiutamaduni.

Anasema ushirika huu, umegawanyika katika aina tofauti kulingana na mahitaji ya jamii husika miongoni mwao ni ushirika wa nyumba, umwagiliaji, wavuvi, walaji, Akiba na Mikopo (SACCOS), anasema Haule.

Anaeleza kuwa ushirika upo duniani tangu miaka 160 iliyopita ambapo pia umeenea kwenye nchi zaidi ya 94 Tanzania ikiwamo huku ukiwa na muunganiko wa watu zaidi ya milioni 800 duniani kote.

Desemba 2, mwaka 1992 Baraza la Umoja wa Mataifa kupitia azimio namba 47/90 lilitambua rasmi siku ya ushirika duniani.

> " 2018 mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Kassim Majaliwa, tulimpa kilio kuomba serikali iturejeshee zilikuwa mali za ushirika ili zirudi kwetu," anasema Haule.

ELIMU

## NA MWANDISHI WETU

SIKU YA CHAKULA DUNIANI

# Walaji 'msichukulie mambo poa' mhakikishe mnachokula salama




Matunda huwekwa chini masokoni bila uangalizi wala onyo la maofisa afya hivyo kuwa kitisho kwa usalama wa vyakula. **PICHA MTANDAO.**

JANA Juni 7, ni siku muhimu ya uhai wa mwanadamu, ndiyo wakati ambao kila mwaka mataifa yanaadhimisha Siku ya Usalama wa Chakula Duniani.

Usalama wa chakula ni muhimu kwa kuwa ndiyo uhai na iwapo mtu atakula kitu chenye madhara, athari zake zinagusa hatima ya maisha yake, ndiyo sababu ulinzi na usalama wa kile kinacholiwa ni suala mtambuka linalohitaji mchango wa wadau wote kuhakikisha kuwa afya ya mlaji inalindwa.

Ili kuwa na chakula salama kila mmoja anawajibu wa kutekeleza katika nafasi yake kuhakikisha kwamba chakula kinakuwa salama na kwa kutambua hilo, kuanzia mwaka 2019 dunia ilianza kuadhimisha Siku ya Usalama wa Chakula Duniani, inayoadhimishwa kila mwaka ifikapo Juni 7.

Mwaka huu yatakuwa maadhimisho ya tatu tangu kupitishwa kwa Azimio namba 73/250 na Mkutano Mkuu wa Afya wa Umoja wa Mataifa (World Health Assembly) uliofanyika 2018.

Kwa mwaka huu kauli mbiu ni: "Chakula salama leo kwa afya njema kesho," ikimaanisha mtu asipopata chakula salama leo, kesho afya yake inaweza kuathirika. Hii ni pamoja na uwezekano wa kupata magonjwa ndani ya muda mfupi au mrefu kutegemeana na vichafuzi katika vyakula.

Vyakula huweza kuchafuliwa na vitu vingi, vikiwamo vimelea vya magonjwa, kemikali za sumu na vitu vigumu kama mawe, mifupa na takataka nyingine na kwa mantiki hiyo, endapo mtu akila chakula kilichochafuliwa na vimelea vya magonjwa, huweza kuugua tumbo, kuhara au kuhara damu . Halikadhalika, akila kilichochafuliwa na kemikali za sumu huweza kupelekea kuugua na hata kupoteza maisha. Aidha, madhara yatokanayo na uchafuzi wa chakula ni makubwa, ikiwa kifo endapo muathirika hatapata tiba sahihi na kwa wakati.

Ni kwa kuona umuhimu wa usalama wa chakula kwa afya ya jamii ndiyo maana serikali inatekeleza jukumu la kudhibiti usalama wa chakula kinachouzwa katika masoko ya Tanzania, jukumu linalofanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Ofisa Usalama wa Chakula Mwandamizi wa TBS, Imakulata Justin, anafafanua kwamba kila mmoja katika mnyororo wa chakula anao wajibu kuhakikisha usalama huo kuanzia kwa mzalishaji anayekitoa shambani au majini, msafirishaji, muuzaji, mlaji na serikali.

### KWA WAZALISHAJI

Imakulata anasema wajibu wa mzalishaji ni kuzalisha chakula salama shambani, pia wanyama wanaofugwa kwa ajili ya chakula wanaozalisha mayai, nyama na maziwa wafugwe kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji.

Halikadhalika, kanuni bora za kilimo ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula kitokanacho na mimea, mfano nafaka, mboga za majani. Jukumu hili hutekelezwa na wazalishaji, ambao hupewa msaada wa kitaalam kutoka kwa maofisa ugani -ufugaji.

Wasafirisha, wafanyabiashara, wahifadhi kwa upande wa wasafirishaji na wafanyabiashara anasema wanalo jukumu la kuweka chakula katika hali ambayo haitasababisha uchafuzi na hivyo kuhatarisha usalama wake, hivyo kuathiri afya ya mlaji.

"Kwa hiyo chakula kisafirishwe au kuwekwa katika hali stahiki, kwa maana kama kinatakiwa kuwa katika mnyororo wa baridi basi hali ya usafirishaji au uhifadhi izingatiwe ili kuepuka uchafuzi. Lakini pia vyakula vingine hutakiwa kuhifadhiwa sehemu ambayo haina mwanga, visipigwe jua, visipate hali ya unyevu," anasema na kusisitiza.

"Mazingira ya kubebea chakula yanatakiwa yasiwe hatarishi kuanzia kuhifadhiwa au kusafirisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine, yasiwe ni mazingira ya kufanya usalama wa chakula ukawa wa kutiliwa mashaka."

### MNUNUZI AU MLAJI?

Aidha, Imakulata, anaainisha kuwa mlaji analo jukumu la kuhakikisha kuwa chakula anachonunua au kutayarisha ni salama. Anasema mlaji au

> "Mfanyabiashara anatakiwa kujua kwamba kama kitu kimepita muda wake wa matumizi hakitakiwi kuuzwa kwa matumizi ya binadamu, lakini na mnunuzi kwa maana ya mlaji wa mwisho na yeye ana nafasi yake kuhakikisha kile anachonunua ni salama kwa afya yake," anaeleza Imakulata na kuongeza:

mnunuzi wa mwisho ana wajibu wa kuhakikisha kuwa chakula anachokula ni salama. "Unakwenda sokoni kununua mahindi, unanunua yapi? Unaangalia kama hayajaoza, yamechambuliwa vizuri na yapo kwenye chombo safi.

Kwenye kunanunua matunda yamewekwaje sokoni? Yamerushwa tu chini au kwenye kichanja? Vile vile unaponunua mboga unatakiwa kuangalia kama mazingira ni salama," anakumbusha Imakulata.

### VYAKULA VYA VIWANDA

Kwa upande huu Ofisa wa TBS, anasema watumiaji wanatakiwa kusoma taarifa zilizopo kwenye vifungashio ili kujiridhisha kama vyakula hivyo havijapita muda wake wa matumizi au kuharibika kwa mwonekano.

Anasisitiza kwamba mlaji wa mwisho anawajibika kujihakikishia kile anachonunua kwa ajili ya kula au kuandaa kwa familia ni salama, akitoa mfano kwamba hata pale mtu anapokwenda kula kwenye mgahawa, lazima ajiridhishe kama mazingira ni safi ili mwisho uwe kila anachokula ni salama kwa afya yake.

### JUKUMU LA SERIKALI

Kwa upande wa shirika hilo, Imakulata anasema ili kuhakikisha usalama wa chakula, TBS pamoja na mambo mengine huandaa viwango vya bidhaa za chakula, kufanya ukaguzi katika viwanda, soko pamoja na udhibiti wa bidhaa za chakula zinazoingizwa ndani ya nchi ili kuhakikisha usalama wake. Aidha, TBS imekuwa ikitoa elimu kwa umma juu ya masuala ya usalama wa chakula.

Anaongeza kuwa ili kuhakikisha kila mmoja anashiriki kwa nafasi yake kuhakikisha usalama wa chakula, TBS imekuwa ikitoa elimu kwa umma, ikiwa ni pamoja na kuelimisha wajasiriamali na wafanyabiashara wa vyakula.

"Mfanyabiashara anatakiwa kujua kwamba kama kitu kimepita muda wake wa matumizi hakitakiwi kuuzwa kwa matumizi ya binadamu, lakini na mnunuzi kwa maana ya mlaji wa mwisho na yeye ana nafasi yake kuhakikisha kile anachonunua ni salama kwa afya yake," anaeleza Imakulata na kuongeza:


"Wafanyabiashara wamekuwa wakielimishwa juu ya kutochanganya bidhaa za chakula na vitu vingine ambavyo huweza kusababisha uchafuzi katika chakula, kama vile mafuta ya taa, betri na dawa za wanyama, mimea na kemikali."Mpangilio ni lazima uwe ni ule ambao hauna muingiliano na vitu vingine, ambavyo si kwa ajili ya kula."

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Kiswahili Pwani VS Maziwa Makuu

## •Museveni anapotoa somo utafsiri



MBINU za kutafsiri hotuba za viongozi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili zililelekea kukwama kwa kiasi wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano ya mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga.

Shughuli hiyo iliyofanyika Ikulu Dar -es -Salaam, Rais Yoweri Museveni wa Uganda(pichani) , ambaye ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar- es- Salaam na aliyefundisha Chuo cha Ushirika Moshi (sasa Chuo Kikuu Kishiriki) alishangaa baadhi ya tafsiri zinazotumika, na kutoa rai kuhusu maneno stahiki kutoka Uganda, kwa mfano. Ilikuwa ni kuhusu neno 'iron ore,' ambako mtafsiri aliendelea kusema chuma wakati alitakiwa kusema 'chuma chenye udongo'

Angekuwa ni huyu mwandishi ndiye anayetafsiri ingekuwa labda ni rahisi zaidi kusema 'udongo chuma' kwani 'iron ore' ni chuma chenye udongo kinachohitaji kupitishwa kiwandani kitolewe udongo na 'uchafu' mwingine. Museveni alikumbuka kuwa kuna tafsiri ya neno hilo kama 'chuma cha pua' alilosikia wakati huo, akaeleza mshangao wake akahoji kwanini wasichukue maneno mengine, na siyo kuunda na kuendeleza mkanganyiko kama huo.

Kumbe suala hapo ni utamaduni tu wa Kiswahili, unavyotofautiana pwani na jinsi unavyozidi kuingia bara, hadi kufika nchi za jirani ambako misemo na hisia zinabadilika.

Neno 'chuma cha pua' ni tafsiri ya 'steel,' yaani chuma kilichoongezewa nguvu, kwa kuchanganywa na 'vumbi' la 'carbon' kuongeza uimara wa muundo wake kuwa chuma kigumu zaidi. Chuma cha pua ni dhana ya mshangao, kama kusema 'dume la mbegu,' si kwa vile yako yasiyo na mbegu ila aina hiyo ya dume ni tofauti na hayo mengine, wanaita Kiingereza 'pedegree,' yaani inayofikia upeo katika hitaji hilo (la mbegu).

Chuma cha pua ni chuma cha kushangaza kwa ubora wake, ila siyo tu kutengeneza chuma kwa ustadi fulani kiwe cha kushangaza ila kuyabadili maumbile yake kwa kuuongeza mseto wa kikemia.

> Inamaanisha kuwa 'nishati' ni kitu kinachounguza kwa haraka au kwa nguvu, na hiyo inaendana na dhana ya uwepo wa nguvu ya kuunguza kama kielelezo cha 'energy' kwa jumla, ingawa neno la Kiingereza linashiria zaidi 'kipa nguvu' kwa hitaji la kuendesha kitu chochote, iwe ni mashine au mwili wa viumbe hai vinavyohitaji nguvu hiyo ili kuendesha maisha yao.

Kinachofanya iwe ni nahau iliyoendana na mahali ilipotungwa kwa wakati huo ni kuwa mzungumzaji wa Kiswahili kutoka Bara au ndani kabisa ya ukanda wa Maziwa Makuu anaweza asielewe matumizi ya neno 'pua,' kwani kwake yeye ni kiungo cha mwili kinachonusa au kupata hisia ya uwepo wa harufu. Inapotumika pamoja na chuma, kama sifa ya chuma maalum, inakuwa kana kwamba haileti maana inayotarajiwa au inayolengwa.

Kuna eneo jingine lilileta tatizo kiasi tu la tafsiri, mkalimani wa Ikulu akajizuia kumweleza Rais Museveni neno sahihi la Kiswahili ni nini, wakati kiongozi huyo wa Uganda akizungumzia 'energy,' sekta hiyo kwa jumla, akasema 'sijui nini tafsiri ya energy.'

Kwa vile kuna wakati Museveni alitaka awe anafanya tafsiri yake mwenyewe si kwa vile mkalimani alikuwa anakosea ila kwa vile anajua lugha hiyo na alitaka afafanue kiasi fulani akitafsiri mkalimani akaacha atafute hiyo 'energy' ni nini. Jambo hilo likapita bila tafsiri halafu wakaja watu kupiga simu redioni baadaye kukumbushia kuwa ni 'nishati.'

Kuna wakati Museveni alitaja neno la Kiganda. Wakati mkalimani hakutaka kutilia maanani wazo la Museveni kutoa tafsiri yenye ladha ya Kiafrika ya 'iron ore,' jitihada hiyo kwa baadhi ya watu kuhusu 'energy' ilileta swali kuwa hivi neno hili 'nishati' limetokea wapi?

Kuna uwezekano kuwa linatokana na mojawapo ya lugha za makabila , kama si Kiarabu ambacho mwandishi huyo hana msamiati wake, kwani katika Kiingereza 'shati' (shirt) ni vazi na haiwezi kuhamishiwa kwenye 'energy,' yaani nguvu joto ikipimwa.

Ila kwa lugha za asili hasa za pwani inawezekana likapatikana neno kama 'nishati,' kwani kwa Kipare 'nisha' ina maana 'naungua' na kwa lugha ya Kiswahili '...ti' ni kiongezeo cha kukoleza, kwa mfano unasikia 'mtu mweusi ti,' yaani weusi umekolea 'kupita kiasi.'

Inamaanisha kuwa 'nishati' ni kitu kinachounguza kwa haraka au kwa nguvu, na hiyo inaendana na dhana ya uwepo wa nguvu ya kuunguza kama kielelezo cha 'energy' kwa jumla, ingawa neno la Kiingereza linashiria zaidi 'kipa nguvu' kwa hitaji la kuendesha kitu chochote, iwe ni mashine au mwili wa viumbe hai vinavyohitaji nguvu hiyo ili kuendesha maisha yao.

Funzo la kubadilishana hisia kuhusu tafsiri ya maneno ni bayana kuwa kuna hitaji kuwa Kiswahili kitumike maeneo makubwa Afrika Mashariki na kusini linaweza kupata msuguano wa kihisia, kuwa lugha nyigine ziweze kuchangia katika kupata tafsiri ya maneno ya Kiingereza, au ya Kifaransa kwa baadhi ya nchi na hata ya Kireno.

Hata hivyo, mwelekeo wa Rais Museveni ambao unaendana na mtazamo wa wataalamu wa kutafsiri hapa nchini unatofautiana na jinsi kuna wakati lugha kunavyoonekana kuwa watu wanachanganya maneno ya Kiingereza au Kifaransa waliyoyazoea katika maongezi ya aina fulani, huku wakiwa na msamiati wa msingi wa Kiswahili kuwezesha maongezi.

Kunakuwa na Kiswahili cha wanaoongea Kiarabu ukanda wa pwani, wanaoongea Kiingereza kama Kenya na Uganda, au Kifaransa huko Congo, Kireno upande wa Msumbiji, huku baadhi yao waliowahi kuishi Tanzania au walioko mpakani wakiwa na uwezo wa kufuatilia Kiswahilii cha hapa nchini, ambacho kimsingi ni hisia za wakazi wa pwani.



# WFP yaombwa mradi wa udumavu mikoa 3

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge,Kazi,Vijana, Ajira na watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ameliomba Shirika la Chakula Duniani (WFP) kupeleka mradi wa Boresha Lishe kwenye mikoa ya Songwe, Iringa na Ruvuma inayoongoza kwa tatizo la udumavu kwa watoto.

Mhagama aliyasema hayo wilayani humo kwenye hafla ya kukabidhiwa mradi huo uliotekelezwa kwa miaka mitano katika Halmashauri nne za mikoa ya Singida na Dodoma, ambao unatarajia kufikia kikomo kesho.

Alisema licha ya mikoa hiyo kuzalisha chakula kwa wingi, lakini inaongoza kwa tatizo la udumavu na lishe duni.

"Naomba WFP mpeleke huu mradi kwenye mikoa hii ili kusaidia mkakati wa taifa wa lishe awamu ya pili ambao utalenga kutokomeza udumavu nchini," alisema.

Aliongeza: "Kumekuwa na tatizo changamoto kubwa ya udumavu kwa watoto hali inayosababishwa na vyakula kutoandaliwa vizuri, ni muhimu suala hilo

likaangaliwa kwa makini."

Alisema mradi huo umekuwa na mafanikio makubwa kwa mikoa ya Dodoma na Singida na kushauri katika awamu ya pili mradi uangalie mikoa hiyo mitatu.

"Mikoa ya Iringa, Songwe na Ruvuma ni wazalishaji wakubwa wa vyakula lakini hawajui kutengeneza vyakula na kuvitumia vizuri, jambo hililikifanyika kwa umakini udumavu utaondoka nchini," alisema Mhagama.

Alisema mradi huo umefikia wananchi 40,664 ambapo kwa sasa wanajua maana ya lishe bora na kutengeneza vyakula vya makundi matano.

Aidha, alizitaka halmashauri kutoa elimu zaidi ya masuala ya lishe ili kutokomeza udumavu.

Mratibu wa mradi, Alissia Decaterina, alisema lengo la mradi ni kuboresha lishe na kuondoa udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano.

Alisema mradi huo unaendeshwa na WFP kwa kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya na wahisani wengine unalenga kuimarisha upatikanaji na matumizi ya chakula chenye lishe kwa wanawake na watoto.

Hata hivyo, alisema wananchi walionufaika na mradi huo wamewezeshwa kufuga kuku, sungura,kuunda vikundi vya vicoba.

"Wahudumu wa vijiji 124 wamepatiwa baiskeli na vipaza sauti ili kutoa elimu, na tumechimba visima vya maji vifupi 75 na vingine 174 vinachimbwa," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justus Kijazi, alisema mradi huo umewasaidia wananchi kiuchumi kutokana na wengi wao kwasasa kuwa na elimu ya kutengeneza lishe bora.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, alisema atahakikisha mradi huo unakuwa endelevu ili wananchi watengeneze lishe bora kwa watoto.



Wajumbe wa mkutano mkuu wa Chama cha Madereva Serikalini Tanzania (CMST), wakimsikiliza Mwenyekiti wao, Charles Mwaihojo (hayupo pichani),alipokuwa akitoa taarifa ya mwaka ya chama hicho kwenye mkutano mkuu uliofanyika mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA PETER MKWAVILA**

## Watetezi wa haki waiomba serikali kuwatatulia kero

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umeiomba serikali kushughulikia kero za kisheria na kiutendaji zinazowakabili watetezi.

Mratibu wa mtandao huo, Onesmo Olengurumwa, alitoa ombi hilo j kwenye mazungumzo kati ya THRDC na Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi.

Alisema serikali iangalie namna ya kutambua na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na mtandao huo ili kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mratibu huyo alisema watetezi wengi wa haki za binadamu nchini wanaoshughulikia na haki za binadamu wamekuwa wakihusishwa na siasa, jambo ambalo si kweli.

"Serikali bado haijathibitisha mikataba kadhaa muhimu ya kimataifa ikiwa ni pamoja na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu la 1998, na Itifaki ya

Hati ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu, juu ya Haki za Watu wenye Ulemavu barani Afrika kwamba itahakikisha kukuza haki za

kimsingi kwa watu wenye ulemavu na mambo yanayohusiana," alisema.

Kwa upande wake, Waziri Prof.Kabudi aliahidi kuwa serikali itaheshimu na kuzingatia mifumo ya kulinda haki za binadamu kwa mtu mmoja mmoja,makundi na jamii kwa ujumla.

"Sisi kama serikali tuna jukumu la kuweka mazingira rafiki kwa wananchi kufikia vyombo vinavyo simamia haki katika ngazi zote,kulinda haki za kikatiba za wananchi wanaoshiriki katika mijadala mbalimbali inayohusu maendeleo ya taifa lao," alisema.

Aidha, alisema wao kama serikali wamekuwa wakichukua hatua ya kupunguza

mrundikano wa kesi mahakamani ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa wasajili wasaidizi katika Halmashauri zote ili kuratibu na

kutoa msaada wa kisheria katika masuala ya mirathi na ndoa.

# Tulia awahamasisha wanawake kugombea

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, amewataka wanawake kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali ili kuongeza idadi ya viongozi wanawake nchini.

Alisema utashi wa kisasa nchini umekuwa chachu ya kuongezeka na kutoa fursa kwa wanawake kushiriki kwenye uongozi.

Dk. Tulia aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kongamano la kuwajengea uwezo wanawake wabunge ulioandaliwa na Kituo cha Usuluhishi(CRC) kwa kushirikiana na Shirika la Kihabari la Femnet kupitia mradi wa wanawake na uongozi na siasa.

Alisema kupatikana kwa Rais wa kwanza mwanamke Tanzania ni kutokana na utashi wa kisiasa uliopo nchini na uwezo wa Rais Samia Suluhu Hassan alionyesha wakati akiwa Makamu wa Rais.

"Hii ni kuonyesha kwamba mwanamke apewe heshima anayostahili, mwanamke ni kiongozi kuanzia ngazi ya familia, anauwezo wa kuongoza nchi na sasa tuna mfano mzuri tunaoutazama

Alibainisha kuwa vijana wa kike wana fursa ya kubwa ya kujifunza na kufuata nyayo kwa kuanza kumuangalia Rais hadi viongozi wa chini.

Alifafanua kuwa Tanzania imepiga hatua kwa wanawake kuwa kwenye uongozi.

Alisema hata teuzi alizofanya hivi karibuni Rais Samia za Makatibu Tawala wa Mikoa wanawake ni asilimia 46.

"Hii inaonesha tunaendelea kupanda, kwa upande wa mawaziri na manaibu waziri wako 11 kati ya 51 sasa ukichukua na wanawake waliopo bungeni unaweza kuona asilimia iko chini, lakini ukiangalia kwa uwiano ni dhahiri tunapiga hatua," alisema.

Alisema kitakwimu bunge, wanawake hawajaongezeka ambapo wanawake wa majimbo kwa sasa ni 24 wakati bunge lililopita walikuwa 25.

"Idadi ya wabunge wa viti maalum pia haijabadilika iko kwenye wastani wa asilimia 37 hivi, sasa sana imebadilika kutoka chama hiki kwenda chama hiki, lakini asilimia 37 sio kidogo, ni hatua kama nchi, ila Tanzania tulishasonga kufikia hii tangu huko nyuma hivyo tunaonekana kama tumegota hivi."

"Kwa hiyo tunahitaji mjadala mpana wa kuona ni kwa nini tumegota hapo tulipogota na namna ya kutoka hapo tulipogota," alisema.

Aidha, alisema wakati mwingine vyombo vya habari hususani mitandao ya kijamii vinawarudisha nyuma wanawake.

"Kupitia mitandao ya kijamii utakuta mtu yuko mbali anamzungumzia mbunge mwanamke ambaye hata hamfahamu, anamtukana na mamno kama hayo, hali hii inarudisha nyuma mwanamke,"alisema.

Awali, Mwakilishi wa Femnet-Prog, Doroth Otieno, alisema kazi ya taasisi hiyo ni kuongeza idadi ya wanawake katika kushiriki katika siasa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, alisema vyombo vya habari vina jukumu la kubeba na kuinua wanawake katika suala zima la uongozi.

Wakichangia baadhi ya wabunge, walisema jamii inapaswa kuwaamini wanawake kuwa wana uwezo wa kuongoza ili kuwapa nafasi.



## Wanufaika kaya maskini watakiwa kuanzisha miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali, imewataka wanufaika wa Mpango wa Taifa wa kunusuru kaya umaskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuanzisha miradi itakayowasaidia baada ya mradi huo kufikia ukomo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kuwatembelea wanufaika wa mpango huo katika Kijiji cha Mpakani kilichopo Kata ya Ubaruku wilayani humo, ambapo aliwaambia kuwa ipo siku mradi huo utafika mwisho.

Mfune aliwataka wanufaika hao kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku, bata, samaki na shughuli za kilimo ambazo zitawasaidia kujiinua kiuchumi kama ilivyo lengo la mpango.

Alisema baadhi ya wanufaika wamekuwa wakizitumia fedha hizo kinyume cha malengo ya Serikali ikiwamo kunywa pombe na baadhi kuzitumia kwa kununua nguo na anasa zingine.

"Nimeona mwenyewe, wale ambao wameitumia vizuri fursa hii wanaonesha mabadiliko makubwa na nataka na wengine wote wawe hivyo, kuna watu nimepita wamefuga kuku, wamefuga nguruwe, bata na wengine walikuwa hawana uwezo wa kuwa hata na gunia moja la mpunga lakini leo wana mazao ya kutosha," alisema Mfune.

Alisema katika maeneo mengi ambayo alipita alibaini maendeleo makubwa kwa wanufaika na hivyo akawataka kujiendeleza ili baadaye waondolewe kwenye mradi na waingizwe watu wengine.

Alisema miradi ya ufugaji wa kuku ni mizuri kutokana na gharama yake kuwa ndogo huku ikiwa na faida kubwa ikiwemo kuongeza ubora wa lishe kwa familia zao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpakani, Amos Mgongolwa, alimuomba Mkuu wa Wilaya kuwatembelea mara kwa mara wanufaika wa mpango huo ili kubaini matatizo yanayowakabili na kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Alisema katika Kijiji chake kuna baadhi ya watu wanastahili kuingia kwenye mpango huo kutokana na hali zao za kiuchumi na hivyo akawaomba maofisa wa TASAF kufanya uhakiki kwa kuwaondoa walioinuka kiuchumi na kuwaingiza wengine.

# Wanafunzi wote waombewa mikopo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), imeshauriwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wanaojiunga na vyuo vikuu wenye sifa bila kujali shule walizosoma.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Montfort wilayani Mbarali, James Nirapal, wakati wa maonyesho ya mbinu za maarifa na ubunifu uliofanywa na wanafunzi.

Maonyesho hayo pia yalishuhudiwa na wazazi, walezi na wananchi wa Wilaya ya Mbarali.

Nirapal alisema shule binafsi kwa sasa zina hali ni ngumu kiuchumi, kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kuhofia kuwa wakiwapeleka watoto wao kwenye shule hizo watakosa mikopo watakapokuwa wanajiunga na vyuo vikuu.

Alisema ni vyema serikali iangalie vigezo vya kitaaluma badala ya kuzingatia mwanafunzi huyo ametokea shule gani, huku akitolea mfano kuwa kigezo mojawapo cha kuzingatia ni ufaulu mzuri wa mwanafunzi pamoja na hali ya uchumi wa familia.

"Sekta binafsi ni muhimu katika kukuza elimu nchini, tumeona ambavyo imewekeza kwa kuwa na idadi kubwa ya shule, lakini katika miaka ya hivi karibuni hatua ya serikali kuwapa mikopo wanafunzi wanaotoka shule za Serikali, kuna 'discourage' (kukatisha tamaa) sekta binafsi," alisema Nirapal.

Mmoja wa walimu wa shule hiyo, Michael Makoga, alisema yamelenga kuonyesha mbinu za maarifa na ubunifu unaofanywa na wanafunzi wa shule.

Alisema ubunifu huo wa wanafunzi utawafanya wawe na uwezo wa kujitegemea watakapohitimu masomo yao kwa maelezo kuwa ubunifu huo utawasaidia kujiajiri.

Alisema wanafunzi walionyesha namna ya kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shughuli mbalimbali, kufua umeme wa maji, kuandaa mashamba, kufuata maelekezo na mafunzo ya sayansi katika mfumo wa damu na moyo kwa vitendo.

"Pia kwa kuwa kwenye shule yetu tunafanya shughuli ya kilimo na ufugaji ni fursa ya kuwaandaa wanafunzi wetu waweze kuitegemea katika siku za mbeleni kwa kutumia ujuzi wanaoupata wakiwa shuleni hata kama hawatapata ajira kwenye mfumo rasmi," alisema Makoga.

Mkurugenzi Msaidizi wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole, alisema kwenye utoaji wa mikopo bodi inazingatia uhitaji wa mtu anayeomba.

Alisema miongoni mwa vitu wanavyozingatia ni hali ya uchumi wa mzazi au mlezi,hivyo wanaamini mtu ambaye ameweza kulipa gharama kubwa kwenye shule binafsi ana uwezo wa kulipa ada ya chuo kikuu.

"Tunazingatia uhitaji, kama wewe ni mtoto wa waziri au mfanyabiashara na umesoma kwenye shule za serikali hatuwezi kukupa kipaumbele cha mkopo, lakini hata kama umesoma shule binafsi na umefadhiliwa masomo yako tutakuona kwenye vigezo vyetu na tutakupa kipaumbele, sisi tunaangalia zaidi ambao hawana uwezo," alisema Ngole.



Baadhi ya wajasiriamali wilayani Chunya wakiendelea na biashara zao juzi ndani ya soko la Uhindini lililopo Chunya mjini, soko ambalo wanadai halina umeme na hivyo kuwalazimu kufunga biashara zao mapema. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Walimu 900,000 kupandishwa madaraja

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema inakusudia kuwapandisha madaraja zaidi ya walimu 90,000 ambao walikuwa hawajapandishwa kwa muda mrefu.

Lengo limetajwa kuwaongezea morali ya kufanya kazi kwa maelezo kuwa idara ya ualimu ndiyo nguzo ya taifa.

Hayo yalisemwa jijini Mbeya juzi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, wakati wa sherehe ya Usiku wa walimu iliyoandaliwa na Msherehesaji maarufu jijini humo, Mwalimu Edwini Luvanda.

Alisema walimu ndio kundi kubwa zaidi kuliko makundi mengine ya watumishi wa umma kwa maelezo kuwa kwa sasa idadi ya walimu wa shule za serikali ni 264,000 sawa na asilimia 68 ya watumishi wote wa umma.

Alisema vilevile Serikali inakusudia kuendelea kuajiri walimu wengi zaidi ili kuwapunguzia mzigo walimu waliopo na kupunguza tatizo la ajira kwa watu wenye taaluma za ualimu ambao wapo mtaani.

"Mheshimiwa Rais wetu ametuahidi kuongeza ajira kwa walimu ili kuongeza maarifa kwa vijana wetu, lakini pia tutaendelea kuwapandisha madaraja walimu ambao hawakupandishwa katika kipindi chote kilichopita," alisema Silinde.

Alisema Serikali pia inakusudia kuendelea kuboresha mazingira ya elimu kwa kujenga shule mpya zikiwamo shule maalumu za wasichana ambazo zitaanza kidato cha kwanza mpaka cha sita na kwamba zitajengwa katika kila mkoa nchini.

Alisema shule hizo zitakuwa za kisasa na kwa mujibu wa makadirio ya bajeti ni kwamba kila shule itagharimu zaidi ya Sh. Bilioni nne mpaka kukamilika kwake.

Vilevile, alisema katika mwaka wa fedha ujao, Serikali imedhamiria kujenga zaidi ya shule 1,000 kwenye Kata zote ambazo bado hazina shule hizo nchini pamoja na kujenga nyumba za walimu ili wakae karibu na vituo vyao vya kazi.

Katika hatua nyingine, Silinde aliwataka walimu kutoa taarifa katika ofisi yake endapo maofisa watumishi watakuwa wanawanyanyasa.

"Moja kati ya majukumu yetu ni kuwalinda walimu, tutahakikisha tunawalinda kwa gharama yoyote na mimi nitakuwa mstari wa mbele kuwapigania maana hata mimi nimefika hapa kwa sababu ya walimu," alisema Silinde.

Mwandaaji wa sherehe hizo, Luvanda alisema aliamua kuandaa sherehe hizo kwa ajili ya kuwakutanisha walimu pamoja na kuainisha matatizo mbalimbali yanayowakabili kwenye kazi yao.

Alisema walimu wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali kwenye kazi zao ikiwamo kutotendewa haki na baadhi ya viongozi wa Halmashauri hali ambayo wakati mwingine huwa inawakatisha tama.

Aliiomba Serikali kuwawekea mazingira rafiki watumishi wa kada hiyo ya ualimu ili wafanye kazi kwa moyo kwa maelezo kuwa wakati mwingine walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu.

"Walimu ni kundi ambalo tumekuwa tukionekana kama kundi la wanyonge sana, lakini ifahamike kwamba sisi ndio tunakaa na watoto muda mrefu kuliko hata wazazi, sasa tunaomba tupewe heshima yetu," alisema Luvanda.





# BOSCH ya Ujerumani kuwekeza Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya BOSCH Groups ya Ujerumani imesema ipo tayari kuwekeza Zanzibar katika nyanja mbalimbali za uchumi.

Rais wa kampuni hiyo Kanda ya Afrika, Dk. Markus Thill, aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ( Kazi, Uchumi na Uwekezaji), Mudrik Ramadhan Soraga na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaban.

"Tumefanya hivyo katika maeneo mengi barani Afrika kulingana na mahitaji, hili ni jambo la maana zaidi kwani uwekezaji katika rasilimali watu ni bora zaidi kuliko vitu," alisema Dk. Thrill.

Kundi la kampuni ya BOSCH ni miongoni mwa kampuni zinazotoa huduma za teknolojia, ambayo imeajiri zaidi ya watu 375,000

ulimwenguni kote, katika mwaka 2015 ilifanya mauzo ya bidhaa na ujuzi yenye thamani ya Euro bilioni 70.6.

Dk. Thrill pia alitumia nafasi hiyo kupongeza ukarimu wa viongozi wa Zanzibar, huku akieleza kuwa kampuni hiyo mbali ya kuwekeza itatoa mafunzo kwa vijana ili kuwawezesha kuingia katika soko la ajira.

Kwa upande wake Waziri Soraga, alieleza kuwa ili kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya uwekezaji nchini, Serikali imeona vyema kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji.

"Ujio wa kampuni hii (BOSCH) utawavutia wawekezaji wengine kufikiria kuwekeza nchini, wakiamini kwamba watapata huduma stahiki kutokana na uzoefu wake katika uwekezaji ndani na nje ya Afrika," alisemaWaziri Soraga.

Alisema kuwa uwapo wa kampuni zinazolisha vifaa na teknolojia ya kisasa kwenye nchi huchochea kasi na ongezeko la miradi ya uwekezaji, na kuongeza fursa za ajira na ukuaji wa uchumi.

Katika mazungumzo hayo Waziri Shaaban, alisema Zanzibar inahitaji

kampuni kubwa, zitakazowekeza katika viwanda vya teknolojia ya habari na mawasiliano na vipuri vya magari na mitambo, hatua ambayo itaongeza kasi ya ukuaji uchumi na maendeleo ya nchi.

"Ili kukuza weledi na uwezo wa nyanja mbalimbali ni lazima kuwa tayari kualika uwekezaji wa kampuni kubwa na zenye uzoefu mkubwa ili kuimarisha viwanda ambavyo vitazalisha ajira," alisema Waziri Shaaban.

Awali akizungumzia ujio wa kampuni hiyo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya watoa huduma wa sekta ya mafuta na gesi (ZAOGS), Balozi Abdulsamad Abdulrahim, alisema kampuni hiyo iliyowekeza katika nchi mbalimbali ulimwenguni imeonesha nia ya kushirikiana na SMZ katika kutekeleza malengo ya maendeleo ya Zanzibar 2050.

"Kampuni hii tayari imewekeza Euro 230,000 kwenye vifaa vya karakana ya magari jijini Dar es salam, kituo hicho inawezesha upatikanaji wa vifaa na huduma za magari na ujuzi vitu vinavyoweza kuanzishwa hapa Zanzibar na kuajiri vijana wetu," alisema Abdulsamad.



Naibu Spika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma (kulia), akizungumza na Mwakilishi Mkaazi wa UN Women nchini Tanzania, Hodan Addou, alipofika ofisini kwake Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# WHO kutoa chanjo ya corona Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeahidi kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar katika kuhakikisha wananchi wanapatiwa kinga dhidi ya maradhi mbalimbali ya kuambukiza ikiwamo corona na kipindupindu.

Mwakilishi wa WHO nchini Tanzania, Dk.Tigest Ketsela Mengestu, aliyasema hayo wakati akizungumza na Waziri wa Afya Zanzibar ofisini kwake Mnazi Mmoja.

Mazungumzo hayo yalihusu mikakati mbalimbali inayoweza kufanyika ili kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanakuwa salama, ikiwamo jinsi ya kupatiwa chanjo inafanikwa vizuri ili kuwalinda wananchi na mlipuko wa maradhi hayo.

Alisema kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo kati ya wananchi wa Zanzibar na watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani, unaweza kusababisha maambukizi ya maradhi mbalimbali, hivyo ipo haja ya kuhakikisha wananchi wanapatiwa chanjo mapema ili kuwaepusha na athari zinazoweza kujitokeza.

Alisema kuwa katika kufanikisha zoezi la chanjo ya Corona WHO, itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya kusaidia kuboresha vituo vya afya, kuvijengea uwezo wa kuwahudumia wananchi pamoja na kuwapatia vifaa ili kurahisisha zoezi hilo.

Naye Waziri Mazrui alisema utolewaji wa chanjo ya Corona na ugonjwa wa kipindupindu ni hatua muhimu, itasaidia katika kuwaweka wananchi wa Zanzibar salama ili waweze kuendelea na haraki mbalimbali za kujitafutia maisha.

Alisema kutakuwa na chanjo za aina mbili moja ya Corona, hivyo amewataka wananchi kutoa ushirikiano katika kupatiwa chanjo hizo muhimu kwa afya zao.

"Tutawapatia chanjo hiyo wafanyakazi wa afya,wafanyakazi wa viwanja vya ndege, wazee pamoja na wananchi wote na ni muhimu kwao na pia ni salama na ninawaasa wananchi waache kusikiliza maneno ya upotoshaji mitandaoni kwani hayana ukweli wowote," alisema Waziri huyo.

Alieleza kuwa miongoni mwa hatua za awali zitakazo chukuliwa katika kufanikisha hilo ni kutoa elimu kwa wananchi wote wa Zanzibar, ili waelewe umuhimu wa chanjo, ili kufanikisha mkakati huo pamoja na kuwataka wananchi watoe ushirikiano mzuri katika kufanikisha zoezi hilo.

Waziri alisema ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja na ukuaji wa uchumi wa taifa kwa jumla unategemea na uwepo wa afya bora kwa wananchi, hivyo amewataka wananchi kupatiwa chanjo ili kusaidia ukuaji wa uchumi wao na wa taifa kwa ujumla.

Mwakilishi wa WHO upande wa Zanzibar, Dk.Girman Andermichael, alisema shirika linafanya kazi kwa karibu na sekta ya afya Zanzibar kwa muda mrefu na kufanikiwa katika kusaidia miradi mingi ya afya Zanzibar ikiwemo kutoa vifaa na wataalamu.

Alieleza kuwa bado kuna uhitaji wa vifaa tiba katika vituo vingi vya afya Zanzibar, aliahidi kuwa shirika litaendelea kufanya jitihada mbalimbali kwa upande wa Zanzibar katika kuhakikisha chanjo za maradhi yote zinapatikana nchini.

Wakati huo huo, mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia idadi ya Watu Ulimwenguni (UNFPA), Jacqueline Mahon, amemkabidhi Waziri wa afya wa Zanzibar msaada wa vifaa tiba.

Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kupumua kwa ajili ya matibabu ya mama na mtoto, vyenye thamani ya dola 105,124, hatua ambayo itasaidia jitihada za Rais wa Zanzibar katika kuboresha sekta ya afya na kufikia malengo ya maendeleo endelevu na ya kitaifa na kupunguza vifo vya mama na watoto.

# 'Limeni mihogo, na viazi, soko lipo'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa kwenye maeneo ya ardhi yenye mawe wametakiwa kulima mazao ya mihogo na viazi vikuu, kwa kuwa vinahimili ukame, pia lipo soko la uhakika ndani ya nchi na nje.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji,Mifugo na Maliasili, Dk.Soud Nahoda Hassan, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, Abdalla Abasi Wadi.

Katika swali lake Wadi alitaka kujua maendeleo ya kilimo cha zao la mihogo na viazi vikuu, pia juhudi zinazochukuliwa na wizara kuwafikira wakulima kuwapatia utaalamu.

Dk. Nahoda alisema wizara imeanza kuwahamasisha wakulima kulima mazao ya mihogo na viazi vikuu, ambavyo soko lake la ndani na nje limekuwa likiimarika siku hadi siku.

Aidha, alisema kazi kubwa inayofanywa na wataalamu wa wizara ni kuwafikia wakulima kuwapatia ujuzi zaidi pamoja na kuwasaidia kupambana na maradhi yanayoshambuliya mazao hayo.

"Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inayofanywa na wizara ya kilimo kwa sasa ni kuwahamasisha wakulima kulima kitaalamu zaidi mazao ya mizizi, ikiwemo Muhogo na Viazi vikuu ambayo soko lake la ndani na nje ni kubwa," alisema.

Waziri Dk. Nahoda aliahidi kuwatembelea wakulima wa jimbo la Nungwi ambao wanaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya mihogo na viazi katika eneo la ardhi ya mawe ambayo inastahamili ukame.

# Mabucha 23 ya nyamapori yashindwa kujiendesha

**Na Christina Haule, Morogoro**

MAMLAKA ya usimamizi wa wanyamapori Tanzania (TAWA), imesema kuwa kati ya mabucha 31 ya wanyamapori manane pekee ndiyo yanaendelea na biashara hiyo.

Aidha, hali hiyo inatokana na kukosekana kwa nyamapori, na kwamba wengi walifungua mabucha hayo kwa kuamini nyama hizo zitapatikana kwa urahisi kama za mbuzi na ng'ombe.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Misungwi alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari

"Upatikanaji wa nyama za nyamapori ni tofauti na nyama za kawaida zilizozoeleka kwa sababu wanyamapori hupatikana kwa kuwindwa na kwamba mwindaji anaweza akawinda na akamuona mnyama na pia anaweza asimpige au asimkamate sababu nao wanalindwa na Mungu na kufanya zoezi la kupata wanyama hao kutumia muda mrefu,"alisema

Misungwi alisema mpaka sasa ni bucha nane pekee ndizo zinazofanya kazi ambapo tayari wameshawaunganisha wenye bucha na wawindaji wa nyama hizo.

Aidha, aliwataka wananchi wakiwamo wenye bucha kuanzisha mashamba ya kufuga wanyama ambayo yatawasaidia kuvuna kulingana na mahitaji yao kwenye bucha vinginevyo wataendelea kukabiliana na changamoto ya kukosa nyama za kuuza mabuchani mwao.

Kwa mujibu wa Misungwi, wameshaanzisha bustani za wanyama 28 nchini ambazo zitawasaidia wenye bucha na wawekezaji wengine kuwa na wanyama watakaotumia kwenye mabucha na wengine kuendelea kuongezeka.

Alisema mwekezaji anapaswa kupewa kitalu kwa ajili ya kukitumia katika shughuli ya uwindaji wa kitalii na kwamba vitalu hivyo 28 vimetengwa kwa ajili ya kuvutia uwekezaji kupitia biashara ya uwindaji wa kitalii.

Vitalu hivyo na ukubwa wa kilomita za mraba kwenye mabano ni Kitalu cha Selous GR MT1 (305) Rungwe River GCA (996) na Piti OA W kilichopo wilayani Chunya mkoani Mbeya.

Vingine kuwa ni Kizigo GR (E) 2 chenye ukubwa wa kilometa za mraba kilichopo kwenye hifadhi ya Kizigo mkoani Singida na Kitalu cha Lwafi-Nkamba GR (3,088) kilichopo kwenye hifadhi ya Lwafi mkoani Rukwa.



Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Makao Makuu, Bw. James Ntalika, akimwelimisha mfanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea wilayani humo.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uganda kufunga mpaka Alhamisi

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa Uganda, Yoeri Museven, amesema kuwa ifikapo Alhamisi nchi yake itafunga mipaka yake, ili kupunguza kasi kusambaa maambukizi ya corona awamu ya pili.

Aidha, huduma za usafiri kuingia nchini humo zitasitishwa ikiwamo mabasi ya kuingia na kutoka wilaya moja hadi nyingine.

Akizungumza jana na BBC, Rais Yoweri Museveni, alisema uamuzi huo umefikia kutokana na kuongezeka kwa wimbi la pili la virusi vya Corona.

Aidha, nchi hiyo imeshafunga shule zote na kusimamisha shuhuli zote zinazosababisha mikusanyiko kwa kipindi cha siku 42.

Miongoni mwa njia kuu za usafiri wa umma zitakazofungwa ni ndege, treni, teksii na mabasi yanayoingia nchini humo kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Tanzania kupitia njia ya Bukoba katika mpaka wa Mutukula na Nairobi kupitia mpaka maarufu wa Busia.

Alisema hatua hiyo pia itahusisha kufungwa kwa shuhuli za baa na majumba ya sinema sambamba na ibada ya misikitini na makanisa.

"Tumefikia hatua hiyo baada ya wizara ya afya kutangaza visa vipya vinavyotokana na Virusi vya Corona kufikia 1,259 ikiwa ni idadi kubwa zaidi ya maambukizo yaliyorekodiwa kwa siku moja, na vifo tisa tangu Jumapili," alisema.

"Kwenye wimbi hili kiwango cha watu kufariki ni kikubwa kuliko tulivyotarajia na wagonjwa wanaoziidiwa ni wengi, kwenye wimbi la kwanza ilituchukuwa miezi mitatu hadi minne kufikia kuwa na hali mbaya lakini sasa ni wiki mbili tu mambo magumu vifo vimefikia 374, na wangonjwa 52,929," alisema.

Aliongeza kuwa kuongezeka kwa visa vya Virusi vya Corona kuliripotiwa wiki mbili zilizopita na maofisa na walijifunga kwa kuzuiliwa kuzuia vituo vya afya kuzidiwa.

# Mchakato wa kupeleka wajumbe mabunge rasmi

**Na Romana Mallya, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametangaza kuanza kwa mchakato wa wawakilishi kwenye mabunge ya uwakilishi na kuwaeleza wabunge watakaoomba nafasi ya ujumbe wa Tume ya Huduma za Bunge wanatakiwa kuwa na uzoefu na heshima.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma na kueleza kuwa wabunge watapewa taarifa kwenye vishikwambi vyao kuhusu nafasi zinazotakiwa kugombewa na katika mabunge mbalimbali.

Spika Ndugai alitaja nafasi hizo ambazo wanatakiwa watu watano ni Bunge la Afrika (PAP), Jukwaa la wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Mabunge (IPU).

Alisema nafasi zilizowazi nyingine ni wawakilishi katika maziwa makuu na makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge na kusisitiza kuwa nafasi hiyo ni kwa ajili ya watu wanaojiheshimu.

"Hii sio (Kamishna) ya kurukia rukia tu inataka watu waliotulia wenye uzoefu wa kutosha, kwa sababu kuwa mjumbe wa kamisheni ni heshima kubwa sana, siyo ya mchezo mchezo tu hizi nyingine tunaweza kumpeleka mtu yeyote," alisema.

Alisema nafasi hizo zinaombwa kupitia kwenye kamati maalum za vyama vya siasa na kwamba wabunge walio wachache bungeni wataomba kupitia utaratibu wao waliojiwekea.

Spika Ndugai alisema: "Waliowengi mnajua mtakapoomba sasa baada ya michakato yao mwishoni ndiyo Spika ataletewa kumalizia utaratibu ambao tutaufanya hapahapa (bungeni)".

## HABARI KIMATAIFA

# Wafuasi TB Joshua waamini amesinzia, atarudi

**Lagos,** NIGERIA

WAFUASI wa Temitope Balogun Joshua maarufu TB Joshua kiongozi na mwanzilishi wa kanisa la Synagogue Church of All Nations (SCOAN), jana walionekana wakiwa wamekusanyika katika makao makuu ya kanisa hilo, mjini Lagos, wakitumaini amesinzia na atarudi.

Huku raia wengi wa Nigeria na Afrika kwa jumla wanaendelea kumuomboleza TB Joshua, wengi wanamkumbuka kwa utabiri na miujiza yake kwa walioamini.

Licha ya kuwa na wafuasi chungu nzima kutoka mataifa tofauti duniani, pia alikuwa na wakosoaji wengi kutokana na mafunzo ya kanisa lake.

Kifo cha TB Joshua kiliibua maswali mengi huku baadhi ya watu wakitaka kujua kilitokana na nini.

Kanisa la SCOAN halikuthibitisha chanzo cha kifo cha ghafla cha mhubiri huyo, licha ya kurasa zake mitandaoni kuandika taarifa za kifo cha kiongozi wao.

Waumini na watu wanaoishi karibu na kanisa hilo walikusanyika kumuomboleza.

"Alikuwa mtu wa Mungu. Sijawahi kuona mhubiri mkarimu anayewasaidia watu hata kama sio wafuasi wa kanisa lake," Saidat ambaye ni muumini wa dini ya Kiislamu aliiambia BBC.

Nkiru, mmoja wa waombolezaji alisema: Nitamkosa sana. Sijui hili kanisa litaendelea vipi baada ya kifo chake."

**BBC**



Kinamama wakionekana wakiwa na majonzi baada ya kupokea taarifa za kifo cha TB Joshua, wakiomboleza kwenye kanisa la Synagogue Church of All Nations (SCOAN), jana, mjini Lagos, Nigeria. **PICHA: BBC**

# Burkina Faso yaomboleza vifo 160

**Ouagadougou,** BURKINA FASO

BURKINA FASO iko kwenye siku ya tatu za maombolezo ya kitaifa, baada ya umwagikaji mkubwa wa damu uliofanywa na kundi la itikadi kali katika kijiji kimoja.

Takribani watu 160, wakiwamo watoto 20 wamefariki, kwenye mashambulizi yaliyofanywa na kundi la itikadi kali.

Mauaji hayo yalitokea katika eneo la mpaka baina ya nchi hiyo na Mali na Niger.

Mauaji hayo yaliyoripotiwa kwa mara ya kwanza siku ya Jumamosi wiki iliyopita, yakiwa ni makubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa nchini Burkina Faso tangu mwaka 2015 ambako yalitokea katika kijiji kimoja kwenye eneo lenye hali tete ya usalama la Kaskazini mwa nchi hiyo.

Mauaji hayo yalifanyika baada ya watu wengine 14 kuuawa siku ya Ijumaa katika kijiji cha Tadaryat kwenye eneo hilo hilo la Kaskazini ambako waasi wenye kufungamana na mtandao wa Al Qaida na wale wanaojiita Dola la Kiislamu kufanya mashambulizi ya kuwalenga raia.

Taarifa za mwanzo zilizotolewa na vyanzo ndani ya eneo hilo zilisema kwamba, waliouawa ni watu 138, wakati serikali ikisema ni watu 132 waliouawa na kiasi 40 waliojeruhiwa.

**DW**

# Kiongozi Boko Haram athibitishwa kufa

**Lagos,** NIGERIA

IKIWA ni wiki mbili baada ya mapigano makali kati ya makundi hasimu ya kijihadi Kaskazini Mashariki mwa Nigeria, kundi la Islamic State Afrika Magharibi (ISWAP), limetangaza kifo cha Abubakar Shekau, kiongozi wa kihistoria wa Boko Haram, katika ujumbe wa sauti.

Ujumbe huo, ulithibitisha kuwa Abubakar Shekau alijilipua na mkanda wake wa vilipuzi ili kukataa kujisalimisha, wakati alipokuwa amezingirwa na wapiganaji wa kundi la ISWAP, katikati ya ngome yake.

Katika sauti ambayo haikuwa na tarehe iliyorekodiwa, sauti inayodhaniwa kuwa ya kiongozi wa ISWAP, Abu Musab al-Barnawi ilisema Shekau alijiua kwa kujilipua na vilipuzi.

Wapiganaji wa ISWAP, walimsaka mbabe huyo wa kivita na kumpatia nafasi ya kutubu na kujiunga nao, al-Barnawi alisema.

"Shekau alipendelea kudhalilishwa katika maisha ya baadaye kuliko kudhalilika duniani," sauti hiyo iliyorekodiwa imesema kupitia njia za kawaida za mawasiliano za ISWAP, aliripoti mwandishi wa RFI, Lagos, Liza Fabbian. Kiongozi huyo wa kijihadi alichagua kujiua mwenyewe kwa kulipuwa mkanda wake wa vilipuzi, badala ya kuanguka mikononi mwa maadui zake.

Mahasimu wa Shekau jana, walifurahi kwa kifo chake na wanalaani katika ujumbe wao wakisema unyama usiokubalika uliofanywa na Abubakar Shekau.

Mfumo wake wa kumwaga damu, hasa dhidi ya raia wa Kiislamu, zilikuwa tayari zimesababisha mgawanyiko wa kundi la Boko Haram, mwaka 2016.

Tangu wakati huo, ISWAP ilipanuwa eneo lake la udhibiti kutoka eneo la Ziwa Chad, hasa ikilenga jeshi la Nigeria, wakati Shekau alikuwa amechukua hatamu za uongozi wa kundi la kihistoria la Boko Haram kutoka makao yake makuu katika wa Sambisa. Shekau aliripotiwa kufariki mwezi uliopita na awali alishawahi kuripotiwa kuuawa. Boko Haram wala serikali ya Nigeria haijathibitisha kifo chake.

**RFI**

# Harry,Meghan wamkaribisha mtoto wa pili

**California,** MAREKANI

MWANAMFALME Harry Mtawala wa Sussex na mke wake Meghan, wametangaza kuzaliwa kwa mtoto wao wa pili, msichana.

Lilibet "Lili" Diana Mountbatten-Windsor, alizaliwa mwishoni mwa wiki, Ijumaa asubuhi katika hospitali ya Santa Barbara, California.

Mama na mtoto wako katika hali nzuri ya kiafya, ilisema taarifa ya wanandoa hao.

Kasri la Buckingham ilisema: Malkia, Mwanamfalme wa Wales na Duchess wa Cornwall na mtawala wa Cambridge na mkewe, wamefahamishwa taarifa hizo."

Mwanamfalme Harry na Meghan, walisema wamempatia mtoto wao wa pili jina la Lilibet ambalo ni jina la utani la Familia ya Kifalme kwa Malkia.

Jina lake la kati, Diana, lilichaguliwa kumuenzi bibi yake mpendwa mtoto huyo, Malkia wa Wales, Princess Diana.

**BBC**

# Huawei yazindua bidhaa mpya HarmonyOS 2

**Shenzhen,** CHINA

KAMPUNI ya Huawei imezindua simu mpya za mkononi saa pamoja na kompyuta vinavyotumia mfumo wake bora wa kiuendeshaji uitwao HarmonyOS 2.

Mfumo huo, utawapa wateja wake huduma bora na zinazoweza kujiendesha kutokana na matumizi ya mtu katika nyakati tofauti.

Mbali na mfumo huo, HUAWEI pia imetoa matoleo mapya ya Mate 40, Mate X2, Watch series 3 na MatePad Pro.

"Kimoja kama vyote, vyote kama kimoja. Tunaishi kwenye dunia ambayo vitu vyote vimeunganishwa na vinaweza kujiendesha. Hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuukwepa mfumo huu," alisema Richard Yu, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo.

Katika hafla ya uzinduzi huo iliyofanyika jana, Huawei ilizindua FreeBuds 4, earphones za teknolojia ya kisasa vyenye uwezo wa kuzuia kelele za nje, vikiunganishwa na simu kwa mfumo wa bluetooth.

Kampuni hiyo pia ilizindua vifaa viwili ya kuongoza vyenye ubora wa juu ambavyo ni MateView na MateView GT.

"HarmonyOS imetengenezwa kushughulikia tatizo hilo. Mfumo huu hutoa lugha ya kawaida kwa vifaa mbalimbali ili viweze kuunganishwa pamoja na kushirikiana, huku ikiwapa watumiaji ubora, ufarisi na usalama wa hali ya juu."



# HAALAND

## SASA SOKONI KWA EURO MILIONI 200

**DORTMUND, Ujrumani**

KLABU ya Borussia Dortmund inataka kiasi cha Euro milioni 200 ili kumuachia straika wake, Erling Haaland, kwa mujibu wa AS.

Haaland ni jina linalotajwa sana wakati huu wa dirisha la usajili la majira ya joto na amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa.

Amekuwa na mafanikio makubwa tangu atue hapo Dortmund, na kufanya klabu kubwa za Ulaya kumtolea macho.

Wakati kukiwa na uvumi mwingi kuhusu majaliwa yake, Dortmund wamekuwa wakipambana kuhakikisha wanambakiza raia huyo wa Norway.

Haaland amekuwa akihusishwa na Real Madrid, Manchester City, Barcelona, Paris Saint-Germain, Manchester United, Juventus, Liverpool, Chelsea na Bayern Munich.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Dortmund imeweka wazi kwamba, inataka mezani kiasi cha Euro milioni 200 kwa timu yoyote itakayotaka kuipata saini ya nyota huyo.

Kiasi hicho cha fedha kimepanda kutoka kile cha awali cha Euro milioni 180 walizokuwa wakitaka Dortmund ili kumuachia mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

## WIJNALDUM AOTA MBAWA BARCELONA

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imefikia makubaliano na kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum, kwa mujibu wa Jarida la France Football.

Barcelona ilikuwa na makubaliano ya maneno na Wijnaldum kumpa mkataba wa hadi hadi Juni 2024 na alitarajiwa kukamilishwa usajili wake siku chache zijazo.

Bodi ya Barça pia ilikuwa imepanga kuandaa vipimo vya matibabu katika kambi ya timu ya Taifa ya Uholanzi wiki ijayo, na kisha kutangaza kumsajili.

Lakini kwa mujibu wa ripoti hiyo, PSG ilijiunga na mbio hizo katika siku tatu zilizopita ikitoa mshahara mara mbili zaidi ikilinganishwa na ofa ya Barcelona na kumpa mkataba hadi Juni 2024.

Wijnaldum alikuwa amebakiza hatua moja kujiunga na Barça, lakini baada ya hali kubadilika aliamua tu kukubali kutua PSG.

Kwa sasa mchezaji huyo anatarajiwa kujiunga na PSG na mkataba unatarajiwa kusainiwa mapema wiki ijayo kukamilisha kandarasi hiyo ya miaka mitatu.

## KANTE: SIFIKIRII KABISA KUHUSU BALLON D'OR

**PARIS, Ufaransa**

N'GOLO Kante anaamini uvumi wa kumhusisha yeye na tuzo ya Ballon d'Or ni jambo la kawaida, lakini yeye akili yake ni kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kutoka kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia dhidi ya Manchester City na kuisaidia Chelsea kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kante amekuwa akitajwa kwamba anastahili kushinda tuzo ya Ballon d'Or.

Lakini Kante mwenyewe amebainisha "sifikiri" huku akiwaambia waandishi wa habari Jumapili: "Ninachokisikia kinanigusa, lakini najaribu kufanya kile ambacho nafanya mara zote: kuwa kawaida na kuisaidia timu katika ubora wangu dimbani. Kama watu itawafurahisha sana, ni bora zaidi."

Alipoulizwa kama anatarajia kushinda tuzo ya Ballon d'Or, Kante alisema: "Ni haraka sana kuzungumzia hilo kwa sasa.

"Ndio kwanza tupo katikati ya mwaka na kuna miezi sita mingine ya kumaliza mwaka, kuna mashindano mengi ya kucheza, na haisaidii kusema kwamba nastahili hiyo kwa sasa.

"Miaka iliyopita nilikuwa kwenye 10 bora, hiyo ilikuwa mara ya kwanza na ilinifanya niwe na furaha.

"Kushinda hiyo itakuwa habari nyingine."

Ilikuwa Desemba mwaka 2017 wakati Kante alipoingia kwenye 10-bora na kumaliza nafasi ya nane katika kura.

## HABARI MICHEZO



# ARSENAL

## WAMKOSA BUENDIA, ATUA VILLA

**LONDON, England**

ASTON Villa wamekubali kulipa dau la pauni milioni 33 ambalo ni rekodi ya klabu hiyo kwa ajili ya kupata saini ya kiungo, Emiliano Buendia kutoka Norwich City.

Buendia mwenye umri wa miaka 24, ameshakamilisha vipimo vya afya akiwa kwao na timu ya Taifa ya Argentina inayojiandaa na michuano ya Copa Amerika.

Ada hiyo ambayo pia itakuwa rekodi ya mauzo kwa Norwich ambao walikataa ofa ya Arsenal na inaweza kuongezeka hadi kufikia pauni milioni 40.

Arsenal walikataa kutoa ofa ya pauni milioni 30 kupata saini ya kiungo huyo wakitaka kupunguziwa bei.

Lakini Villa ikatumia mwanya huo na kujitosa kwenye kinyang'anyiro hicho na kukamilisha dili hilo.

Buendia alifunga mabao 15 na pasi za mwisho 16 msimu wa 2020-2021 kwenye Ligi Daraja la Kwanza na sasa Norwich imepanda Ligi Kuu England.

## BARCA HAINA HARAKA NA FATI

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA haina haraka ya kumwongezea mkataba nyota wao kinda, Ansu Fati, ambao wa sasa unamalizika mwaka 2022.

Kwa mujibu wa AS, Barcelona kwa sasa kipaumbele chao ni kuingia sokoni kusajili wachezaji wapya katika wiki chache zijazo.

Mazungumzo kati ya pande hizo mbili juu ya uwezekano wa kuongeza mkataba mpya yalianza miezi iliyopita na yanaonekana kuwa katika njia sahihi.

Barcelona inamuona Fati kama sehemu muhimu ya siku zijazo za klabu na wana matumaini juu ya matokeo ya mazungumzo na wawakilishi wa kijana huyo.

Fati kwa sasa anaendelea kuuguza jeraha kubwa la goti lililomlazimisha kufanyiwa upasuaji mara kadhaa wakati wa msimu uliopita baada ya kuumia Novemba 7, mwaka jana. "Mkataba wake mpya umecheleweshwa, lakini Barcelona hawajafikiria hali yoyote ambayo itamfanya Fati aondoke klabuni hapo," liliripoti AS.

'Blaugrana' hao wamewekka kipaumbele katika kuweka saini kwa wachezaji ambao wapo huru kwa sasa, mmoja wapo akiwa Memphis Depay ambaye mkataba wake umemamlizika kule Lyon.

## CHELSEA TAA YA KIJANI KWA COMAN

**LONDON, England**

CHELSEA na Manchester United wamekuwa wakihusishwa na kuhitaji saini ya winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman, ambaye anaweza kuwekwa sokoni na mabingwa hao wa kihistoria kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kwa mujibu wa ripoti, Chelsea ipo kwenye sehemu nzuri zaidi ya kunyakuwa saini ya winga huyo mwenye ujuzi wa kutosha kwa sababu kadhaa.

Kwanza inadaiwa kocha wa Chelsea kuwa na ukaribu na viongozi wa Bayern Munich, hivyo haitokuwa ngumu sana kwa 'The Blues' kupata saini ya Coman pindi tu atakapowekwa sokoni.

Suala la fedha, United wamekuwa wakihangaika sana kwenye kuboresha kikosi chao, jina la Jadon Sancho bado linaumiza vichwa vya mabosi wengi pale Old Trafford, hivyo Euro milioni 55 zinazotakiwa na Bayern zinaweza kuwa nyingi sana kwao. Chelsea itanufaika sana na usajili wa Coman pale Stamford Bridge, hii ni kutokana na ukweli kuwa wachezaji wao kama Hakim Ziyech kutokuwa na mchezo mzuri.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE HAUZWI NA HAONDOKI BURE - PSG

●●●Atakwenda wapi? Klabu gani itashindana na PSG leo hii? Hii ni nchi yake…

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi, amesisitiza Kylian Mbappe kamwe hatauzwa au kuondoka kwa uhamisho huru wakati huu uvumi ukiendelea kumhusisha na Real Madrid.

Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG kwenda kwa miamba ya LaLiga, Real Madrid, huku wababe wa Ligi Kuu England, Liverpool pia wakihusishwa naye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake utamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22, lakini PSG wanajiamini majaliwa ya Mbappe yapo hapo kwenye mji mkuu wa Ufaransa.

Na sasa Al-Khelaifi ameibuka na kuweka wazi kuwa uvumi unaondelea kuhusu mchezaji huyo wakati huu wa kuelekea michuano ya Euro 2020 hauna maana yoyote.

"Nitakuwa wazi kabisa," alisema Al-Khelaifi akiliambia L'Equipe.

"Mbappe anabakia Paris.

"Kamwe hatutamuuza na hataondoka kwa uhamisho huru. Mbappe ana kila kitu anachohitaji hapa Paris.

"Atakwenda wapi? Klabu gani, likija suala la malengo, nani atashindana na PSG leo hii?

"Kitu pekee ninachoweza kusema kwa sasa, kila kitu kinakwenda sawa na nina matumaini tunaweza kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya.

"Hii ni Paris na hii ni nchi yake.

"Ana malengo, si tu kucheza soka, lakini pia kuipaisha Ligue 1, nchi yake na mji wake mkuu."

## KWA UFUPI

**VILLA YAJIPANGA KWA JAMES**

KLABU ya Aston Villa iko tayari kumnunua kiungo wa kati wa Southampton na England, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 26, siku moja baada ya kukubali kuvunja rekodi ya usajili wa klabu hiyo kumsainisha kiungo wa kati mwenzake Emiliano Buendia kutoka Norwich City. ***(Guardian)***

**BEI YA HAALAND HII HAPA**

ITAGHARIMU kiasi cha Euro milioni 200 kumnunua mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, kutoka Borussia Dortmund msimu huu. ***(AS)***

**NEVES KUTUA ARSENAL**

KLABU ya Wolves inajiandaa kupokea ofa ya Arsenal wiki hii ili kumuachia kiungo wao wa kati, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ureno. ***(Mail)***

**BARCA WAMTAKA LAPORTE**

BARCELONA wamefufua tena mpango wa kumsaka mlinzi wa Manchester City, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 27, na huenda wakamtoa Sergi Roberto mwenye miaka 29, kama sehemu ya kufanikisha mkataba. ***(Sport)***

**GIROUD ANUKIA MILAN**

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, huenda akajiunga na AC Milan, licha ya Chelsea kutangaza mpango wa kumwongezea mkataba wa mwaka mmoja wiki iliopita. ***(Goal)***

**TRIPPIER AWANIWA ARSENAL**

ARSENAL inapanga kuingia kwenye mbio moja na Manchester United kumwania mlinzi wa pembeni wa England na Atletico Madrid, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30. ***(Metro)***

**BARCA WAKUBALI YAISHE**

BARCELONA wameamua kutoongeza ofa ya Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, baada ya Paris St-Germain kuongeza mara mbili marupurupu ya ofa iliyotolewa na Barca. Kiungo huyo wa kati wa Uholanzi, ambaye yuko huru kuondoka Liverpool, anajiandaa kusaini mkataba wa miaka mitatu na PSG. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

**JUVE WAMTAKA DEPAY**

JUVENTUS huenda wakajaribu kuwania kumsajili mchezaji mwingine anayelengwa na Barcelona, mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 27, ambaye anajiandaa kuondoka Lyon kwa uhamisho huru. ***(Mundo Deportivo)***

**BETIS YAMUWANIA BALBUENA**

REAL Betis wamepiga hatua katika mazungumzo yao na mlinzi wa Paraguay, Fabian Balbuena mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake katika klabu ya West Ham unaelekea kumalizika. ***(Mundo Deportivo)***

**PARATICI KUTUA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur itathibitisha uteuzi wa mkurugenzi wa soka wa zamani wa Juventus, Fabio Paratici msimu huu, baada ya juhudi zao za kumpata Antonio Conte kugonga mwamba. ***(Mirror)***

**SARRI HUYOOO LAZIO**

KLABU ya Lazio huenda ikamchukua kocha wa zamani wa Juventus na Chelsea, Maurizio Sarri mwenye umri wa miaka 62. ***(Corriere dello Sport)***

HABARI MICHEZO

# DUBE, LWANDAMINA MCHEZAJI, KOCHA BORA LIGI KUU BARA MEI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI na Kocha Mkuu wa Azam FC, Prince Dube na George Lwandamina, wamechaguliwa kuwa mchezaji bora na kocha bora wa mwezi Mei wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa msimu wa 2020/21.

Dube na Lwandamina walitwaa tuzo hiyo baada ya kuwashinda wenzao walioingia nao fainali kwa mwezi huo, katika uchambuzi uliofanywa mwishoni mwa wiki iliyopita na Kamati ya Tuzo za VPL, kutokana na mapendekezo ya makocha waliopo viwanja mbalimbali nchini.

Katika kinyang'anyiro hicho, Dude aliwashinda mchezaji wa Kagera Sugar, Erick Mwijage pamoja na kipa wa Yanga, Metacha Mnata ambao walikuwa na kiwango kizuri kwa mwezi huo.

Dube alikuwa na mchango mkubwa kwa timu yake kwa Mei na kuonyesha kiwango cha kuvutia akifunga mabao mawili na kuhusika katika bao moja, wakati Azam ikicheza michezo miwili na kushinda yote.

Hiyo ni mara ya pili kwa Dube kutwaa tuzo hiyo, ambapo mara ya kwanza ilikuwa Septemba mwaka jana, pia Aprili yeye na Raphael Daudi wa Ihefu FC waliingia fainali lakini wakashindwa na kiungo Clatous Chama wa Simba.

Kwa upande wa Lwandamina alitwaa tuzo hiyo baada ya kuiongoza Azam kushinda michezo hiyo miwili, ambapo ilizifunga KMC mabao 2-1 na Biashara United 2-0 na kuendelea kubaki nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu, hivyo kuwashinda kocha Francis Baraza wa Kagera Sugar na Abdallah Mohamed wa JKT Tanzania.

Wachezaji ambao wametwaa tuzo hiyo kwa msimu huu na miezi yao katika mabano ni Prince Dube (Septemba), Mukoko Tonombe wa Yanga (Oktoba), John Bocco wa Simba (Novemba), Said Ntibazonkiza wa Yanga (Desemba), Deogratius Mafie wa Biashara United (Januari), Anuary Jabir wa Dodoma Jiji (Februari), Luis Miquissone wa Simba (Machi) na Clatous Chama wa Simba (Aprili).

Makocha waliotwaa tuzo hiyo ni Aristica Cioaba aliyekuwa Azam (Septemba), Cedric Kaze aliyekuwa Yanga (Oktoba na Desemba), Boniface Mkwassa wa Ruvu Shooting (Novemba), Francis Baraza aliyekuwa Biashara (Januari), Zuberi Katwila wa Ihefu (Februari), Mohammed Badru wa Gwambina (Machi) na Didier Gomes wa Simba (Aprili).

Wakati huo huo, Kamati ya Tuzo imemchagua Meneja wa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam, Sikitu Kilakala, kuwa mshindi wa Tuzo ya Meneja Bora wa Uwanja kwa mwezi wa Mei. Ushindi wa Meneja huyo umetokana na kufanya kwake vizuri katika menejimenti ya matukio ya michezo iliyofanyika kwenye uwanja huo kwa Mei pamoja na masuala yanayohusu miundombinu uwanjani.

## MBIO ZA MAGUNIA...




Walimu wa Shule ya Msingi Al- Hekma (Kushoto), na wazazi wa watoto wanaosoma shule hiyo wakishindana kukimbia kwa magunia katika Tamasha la Siku ya Mtoto wa Azam, lililofanyika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uhamiaji, Jang'ombe ni vita kupanda Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MBIO za kuwania kupanda Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao zimeendelea kupamba moto baada ya upepo wa heri kuvuma kwa timu kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Timu hizo ni Uhamiaji FC, ambayo ni kinara wa ligi hiyo ikiwa na alama 41 huku ikifuatiwa kwa karibu na Taifa Jang'ombe inayoshika nafasi ya pili ikiwa na pointi zake 40 baada ya juzi kushinda mabao 2-1 dhidi ya Dulla Boys.

Tofauti hiyo ya alama moja kati ya timu hizo imeongeza ushindani na mvuto kwenye ligi hiyo huku mashabiki wakizidi kuhamasika kwa kufuatilia kwa karibu kutaka kujua ipi itapanda daraja msimu huu.

Ligi hiyo kwa sasa kila timu imebakisha michezo miwili kabla ya kufikia ukingoni kwa msimu huu.

Kwa upande wa Taifa Jang'ombe imebakisha mchezo dhidi ya Mchangani United na Gulioni FC, wakati Uhamiaji FC kibarua kilichopo mbele yake kikiwa dhidi ya Ngome na New King.

Kilichobaki kwa sasa ni kila timu kupigana kupata ushindi huku ikimuombea mwenzake kupoteza ama kupata sare moja kati ya mechi hizo mbili.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, makocha wa timu hizo, kila mmoja alisema lengo lake kubwa ni kuona timu yake inacheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Kwa upande wa Kocha wa Uhamiaji FC, Amaan Khamis "Gulity", alisema atahakikisha anashinda michezo yote iliyobakia ili kuhakikisha lengo hilo linatimia.

Kocha wa Taifa Jang'ombe, Mustafa Hassan, yeye alisema anahitaji pia kushinda michezo yote ingawa anajua itakuwa vigumu kutokana na upinzani uliopo kati ya timu zinazopambana kuepuka kushuka faraja na zinazowania kupanda.

# Leseni zaidi za 'Kubeti' kuendelea kutolewa

**Na Romana Mallya, DODOMA**

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema katika mwaka fedha 2021/22, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha itaendelea kutoa leseni 11,367 kwa waendesha michezo ya kubahatisha.

Waziri wa wizara hiyo, Dk. Mwigulu Nchemba, ndiye aliyetoa kauli hiyo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo iliidhinishiwa matumizi ya Sh. trilioni 12.9.

**Alisema katika leseni hizo, mpya ni 7,408 na zi takazohuishwa ni 3,959.**

Alisema watafanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 76 na kutoa elimu ili ushiriki katika michezo hiyo uwe ni wa kiasi na wa kujitambua.

## Malale aangazia historia kwa Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, amesema anaendelea kukiandaa kikosi chake kuelekea michezo iliyobaki hususan dhidi ya Simba ambayo imekuwa bora zaidi msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema mchezo wao dhidi ya Simba utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wapinzani wao, hivyo wanapaswa kujipanga vizuri kukabiliana nao ili kuwa timu ya tatu kuwafunga 'Wekundu wa Msimbazi' hao kwa msimu huu.

Alisema msimu huu anahitaji kuwa sehemu ya historia kwamba ni miongoni mwa timu ya tatu kuifunga Simba, hali ambayo inamlazimu kuwaandaa wachezaji wake kwa kuwapa mbinu mbadala huku akiwataka kila mchezaji kujitoa katika mchezo huo.

"Tunahitaji kushinda mechi zetu zote ili tuendelea kuwapo katika nafasi nzuri, ikiwamo dhidi ya Simba ambao tutacheza nao karibuni, tunatambua ubora wa wapinzani wetu hao, yeyote anayesema Simba ni ya kawaida anadanganya, lazima ujiandae kisaokolojia na uwanjani kupambana nao ili kupata pointi," alisema.

# Michezo

Jumanne Juni 8, 2021

Nipashe




MBAPPE HAUZWI NA HAONDOKI BURE - PSG

HABARI UK 22

HIYO!...



Bondia Logan Paul (Kushoto), akipenyeza ngumi kwa Floyd Mayweather kwenye pambano la raundi nane ambalo halikuwa la ushindani (la maonyesho), lililofanyika jana alifajiri katika Uwanja wa Hard Rock, Miami Gardens nchini Marekani. Katika pambano hilo ambapo hakutangazwa mshindi kwa kuwa halikuwa na jaji, wengi walidhani Paul angepigwa mapema kwa Knock Out (KO), lakini alikomaa na kumaliza raundi zote nane. **PICHA: MTANDAO**

# WACHEZAJI YANGA WAANIKA UDHAIFU

●●●Wataja kilichoiangusha msimu huu huku wakiutaka uongozi sasa kumulika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WACHEZAJI wa zamani wa Yanga wameibuka na kuanika idara zilizoiangusha klabu yao uwanjani msimu huu na kutoa maoni kuelekea dirisha la usajili la msimu ujao.

Wakizungumza jijini Dar es Salaam, wachezaji hao Ramadhani Kampira na Bakari Malima 'Jembe Ulaya', wamesema inasikitisha kuona hakuna mcheza yeyote wa Yanga ambaye yuko kwenye kinyang'anyiro cha kuwania ufungaji bora.

Wachezaji hao wamesema hayo kufuatia kuwapo taarifa ya klabu ya Yanga kutaka kumsajili beki wa kulia wa AS Vita ya DR Congo, Djuma Shaaban.

"Yanga wanatakiwa kuongeza watu wengine wenye uwezo wa kupachika mabao. Kuna matatizo sana sehemu ya ushambuliaji, ingawa katikati kidogo kunatakiwa kufanyike marekebisho, lakini mbele ni matatizo," alisema Jembe Ulaya.

Alishauri kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara itakapomalizika, suala la usajili liwe na watu wengi, hasa wachezaji wa waliowahi kuichezea timu hiyo wahusishwe ili kupata wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kuichezea timu kama hiyo.

"Yanga ilifanya kosa kubwa sana kumuachia David Molinga. Yule ndiyo alionekana kama mzito kwa sababu hajacheza muda mrefu, lakini alikuwa ni mshambuliaji mzuri sana kama angepewa muda, sema mihemko ya mashabiki ikawaingia viongozi wakaachana naye. Hata kama hawatowaondoa mastraika waliopo, lakini watafute wengine," alisema.

Kwa upande wa Kampira, alisema kama wasipoangalia na kufanya usajili kwa makini, Yanga msimu ujao inaweza ikarudi pale pale.

"Mimi nawashauri watoe nafasi kwa wachezaji wa zamani ndiyo watafute wachezaji. Kuna wachezaji wazuri Zambia, DR Congo, lakini nani anakwenda kuwaangalia na kuwaleta. Bado sisi Yanga tuna tatizo kwenye ushambuliaji, hilo ndiyo kwanza lingekuwa kipaumbele kuliko mengine," alisema winga huyo wa zamani.

Katika hatua nyingine kutokana na Ligi Kuu Tanzania Bara kusimama, uongozi wa Klabu ya Yanga umeamua kutafuta mechi za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao wa ligi hiyo dhidi ya Ruvu Shooting.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema uamuzi wa kutafuta mechi za kirafiki unatokana na Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, kuhitaji timu icheza mchezo wa majaribio kabla ya ligi kuendelea.

Alisema wanatarajia ndani ya wiki hii kupata timu moja inayocheza Ligi Kuu ambayo itathibitisha kucheza nao mechi hiyo ya kirafiki ili kuwapa wachezaji wao utimamu wa mwili.

"Ni kweli kocha amefikisha maombi ya kuhitaji mechi za kirafiki, kulingana na timu nyingi za Ligi Daraja la Kwanza kuvunja kambini baada ya ligi yao kumalizika, hivyo tumekuwa na changamoto ya kupata timu ya kucheza nayo. Tuna matumaini ndani ya wiki hii kupata timu ya ligi ambayo tutacheza nayo.

"Mechi hiyo itampa kocha mwanga wa kuona yale aliyokuwa akiyatoa kwenye mazoezi yamefanyiwa kazi, lakini pia kuwapa nafasi wachezaji ambao hawakupata nafasi katika mechi zilizopita za ligi," alisema Mfikirwa.

## SABABU KAHATA KUTEMWA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa Simba, Coastal Union na timu ya Taifa, Taifa Stars, Mohamed Mwameja, amemtaja Francis Kahata kuwa ni mchezaji mzuri, lakini kilichomuondoa ndani ya kikosi hicho ni upungufu kwenye ukabaji.

Mwameja alisema hayo juzi akitoa maoni yake kuhusu Simba kuachana na kiungo huyo mshambuliaji, ambaye amemaliza mkataba wake na klabu hiyo kutomhitaji tena.

Mwameja amesema kuwa Kahata ni mchezaji mzuri kwenye nafasi ya kiungo na amekuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi cha Simba, lakini anavyoona hakuongezwa mkataba kwa sababu wameletwa wachezaji ambao kiuchezaji wako kama yeye, lakini kuna vitu wamemzidi.

"Kahata ni mchezaji mzuri kwa sababu ni mmoja wa wachezaji waliofanya Simba kufika hapa ilipofikia, lakini naona imeamua kuachana naye kwa sababu ukiangalia Simba imeleta tena wachezaji kwenye nafasi anayocheza kama yeye ambao wamemzidi kwenye eneo la ukabaji ambalo yeye ana mapungufu kidogo," alisema Mwameja.

Mwameja alisema katika soka la kisasa, makocha wengi wanapendelea zaidi mchezaji mwenye uwezo pia wa kukaba kama timu ikipoteza mpira, sifa ambazo Kahata zimemuacha kidogo.

Mmoja wa wachezaji ambaye anatajwa na wadau wa soka kuchangia Kahata kuondoka ni Luis Miquissone, ambaye alisajiliwa na kumkuta mchezaji huyo kutoka Kenya, lakini kiwango chake kimekuwa kikubwa zaidi kwenye nafasi ya winga na kiungo mshambuliaji pia.

Miquissone alisajiliwa msimu mmoja na nusu uliopita akitokea UD Songo wa Msumbiji ambako alikuwa akicheza kwa mkopo kutoka Mamelodi Sondowns ya Afrika Kusini, huku Kahata akiwa amesajiliwa misimu miwili iliyopita akitokea Gor Mahia ya Kenya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002